# Nipashe

Jumamosi Novemba 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581127

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT TZS.1,048,875,802 KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU! SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Mwinyi** aitupa hoja ya ACT kuhusu uteuzi wa kigogo ZEC

UKURASA 5



ACHENI KUMKERA MOBETTO

UKURASA 16

# Waathirika ajali ya ndege fidia bil. 400/-

• **Shujaa** Majaliwa atinga bungeni, apewa mamilioni... Ukurasa. 2



Lori lililobeba mifuko ya saruji likiwa limepinduka baada ya kufeli breki na kusababisha ajali kwa kugonga magari saba katika mteremko wa Barabara ya Wazo, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. Mtu mmoja amefariki na wawili kujeruhiwa vibaya katika ajali hiyo. Picha ndogo: Baadhi ya magari yaliyogongwa na lori hilo. **Habari zaidi Uk. 3. PICHA ZOTE: JOHN BADI**

## Samia ashtuka mifugo kunywa lita 225,000 kila siku Mto Ruvu

UKURASA 2

RIPOTI MAALUM

UKURASA 4

## Wavuvi wanavyouhusisha uhaba wa samaki na dhambi


MICHEZO HASIRA ZA SIMBA KWA IHEFU LEO UK.32

MAONI, KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akibonyeza kitufe kuwasha mtambo wa kutoa maji chini ya ardhi kwenye kisima kirefu cha mita 450 kwa ajili ya kuyapeleka kwenda kwenye tanki kubwa la maji katika eneo la Kigamboni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Waathirika ajali ya ndege fidia bil. 400/-

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

WABUNGE wameitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kuhakikisha abiria waliokuwa katika ndege ya Kampuni ya Precision Air iliyopata ajali mwezi huu mkoani Kagera, kulipwa stahiki zao za bima mapema.

Kwa mujibu wa TIRA, Precision Air ina bima ya dola za Marekani milioni 50 (Sh. bilioni 116.471) kwa ajili ya ndege hiyo na kwa abiria ni zaidi ya dola za Marekani milioni 170 (Sh. bilioni 396).

Ndege hiyo ilianguka kwenye Ziwa Victoria na kusababisha vifo vya abiria 19 huku 24 wakiokolewa na wananchi, hasa wavuvi.

Akizungumza kwenye semina ya masuala ya usalama wa barabarani juzi, Mbunge wa Namtumbo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa, aliagiza wapate bima zao mapema.

"Wote tulishuhudia ajali ile sijui uchunguzi wa nini, haya ndo aliyokuwa anasema Spika inatokea ajali ya gari uzembe ni wa dereva lakini abiria wanashindwa kupata haki zao," alisema.

Aliitaka mamlaka hiyo kusimamia bima iliyokatwa ili iwalipe waathirika wote wa ajali hiyo, wawe wamefariki dunia au wamenusurika.

Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), Charles Mwijage, alihoji: "Abiria waliokuwamo kwenye ndege na kuanguka walifariki dunia na Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) aliona na kila mtu aliona. Uchunguzi ni wa nini badala ya kusema mwezi fulani watu hao watalipwa fidia zao?"

Akitoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali za wabunge, Kamishna wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware alisema abiria hao watalipwa bima na kampuni za ndani na nje ya nchi kulingana na taratibu za kibima zilizopo. Alisema Precision Air ilikata bima halali kwenye kampuni mbalimbali ikiwamo kampuni ya Tanzige na Tanzania Insurance Company.

"Kiasi kilichokuwa insured kwa Precision Air ni dola za Marekani milioni 50 na kwa abiria ni zaidi ya dola za Marekani milioni 170," alibainisha.

Alisema utaratibu wa kibima utachelewa kidogo kutoa fidia kutokana na uchunguzi na taratibu za kibima za kimataifa.

**SHUJAA MAJALIWA**

Katika hatua nyingine, kijana Majaliwa Jackson jana alikuwa miongoni mwa wageni bungeni na kutambulishwa rasmi kama shujaa aliyesaidia kuokoa abiria waliokuwa kwenye ndege hiyo iliyoanguka Ziwa Victoria Novemba 6 mwaka 2022.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson alimtambulisha kijana Majaliwa kwa wabunge jijini Dodoma baada ya kipindi cha Maswali kumalizika mapema jana asubuhi.

Baada ya utambulisho huo huku Spika akimpongeza kijana huyo pamoja na mama yake, baadhi ya wabunge waliomba mwongozo wa kukatwa posho zao ili kumpa zawadi na wengine wakiomba baba yake apongezwe.

Katika mwongozo wa kutaka wabunge wakatwe Sh. 50,000 kutoka kwenye posho zao ili kijana apewe kama zawadi, Dk. Ackson alikataa badala yake akasema kwa mbunge anayetaka kumpa zawadi watoa huduma wa Bunge watapita na kukusanya michango hiyo kutoka kwa mbunge mmoja mmoja.

Kuhusu kumpongeza baba wa kijana huyo, Dk. Tulia alimtaka mbunge aliyeomba mwongozo ampongeze mwenyewe kwa kuwa uamuzi wa Bunge ni kumpongeza mama pekee.

Hoja ya kumpongeza baba yake mzazi kijana huyo ilizua malumbano huku Spika akikataa Bunge kumpongeza baba wa kijana huyo.

Kijana huyo alifika bungeni mapema jana asubuhi kwa mwaliko wa Mbunge wa Bukoba Mjini, Steven Byabato.

Ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu 19 huku wengine wakiokolewa na Majaliwa baada ya kuvunja mlango wa ndege hiyo iliyoanguka ziwani. Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa aliliarifu Bunge jana kuwa kijana huyo ameshapewa nafasi ya kujiunga na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili akapate mafunzo zaidi.

Alisema kijana huyo alipita bungeni jana akiwa njiani kwenda chuoni kwa ajili ya kuanza mafunzo yake ya kijeshi.

Kijana Majaliwa alikabidhiwa Sh. milioni 5.022 zilizochangwa na wabunge kwa ajili yake jana.

***Imeandaliwa na Augusta Njoji na Richard Makore**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
04.10.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Kampuni ya **FM CARGO LTD** inatarajia kusafirisha **(kuanzia tar 13/11/22)** mizigo mipana kutoka **Dar es Salaam kwenda Kigoma** kupitia Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida na Tabora kwa kutumia magari yafuatayo
**T609CXC/T698CCB,T258CHH/T457CHH,T347DYW/T928DYK T480DPZ/T691DPE,T478DPZ/T692DLX,T911CMX/T413CWU**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 22M**
**Upana - mita 4.2M MPAKA 4.86**
**Kimo - mita 5M**
3. Njia itakayotumika: **Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida na Tabora,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117145602


# Samia ashtuka mifugo kunywa lita 225,000 Ruvu

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemshtuka ongezeko la mifugo katika Mto Ruvu linavyosababisha upungufu wa maji huku akibainisha kuwa kuna ng'ombe 5,000 ambao kwa siku wanakunywa lita 225,000.

Kutokana na hali hiyo, amemwagiza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, kudhibiti idadi ya mifugo inayoingia katika mito mbalimbali nchini, ukiwamo Ruvu, ambayo imesababisha upungufu wa maji na uharibifu wa mazingira.

Samia alitoa agizo hilo jana Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mradi wa maji, mitambo ya kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa pamoja na kukabidhi eneo la ardhi kwa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Kidunda.

Alisema kuna zaidi ya ng'ombe 5,000 wameingizwa katika Mto Ruvu, hivyo kusababisha upungufu wa maji huku akibainisha kuwa ng'ombe mmoja anakunywa lita 45 kwa siku.

"Sasa ng'ombe 5,000 wanakunywa kiasi gani mpaka yabaki maji yanayoweza kufika katika mitambo na kusafishwa yafike kwa wananchi?" alihoji.

Rais Samia alisema kuna kazi mbaya inayofanywa katika Mto Ruvu na mito mingine ikiwamo watu kujenga mabwawa ndani ya mito, kuchepusha maji na kusafisha madini.

"Waziri wa Mifugo mkae na kuangalia njia ambazo mifugo yenu itakwenda kutulia mahali. Hii ni kwa nchi nzima siyo Pwani na Dar es Salaam pekee. Mifugo inasambaa ovyo na kuchangia uharibifu wa mazingira," alisema.

"Ardhi inayoikanyaga mifugo 5,000 kwa mara moja kama ni ardhi oevu maana yake hata maji yanaacha kujitengeneza. Lakini si tu ukosefu wa maji, mnapoachia wafugaji kuzunguka Tanzania nzima mnasababisha vifo, mapigano ya wakulima na wafugaji. Tumechoka kusoma hizo ripoti, wamekufa watano visasi vimelipwa. Hii haitasaidia naomba sana muende kusimamia," alisisitiza.

Rais pia aliiagiza Mamlaka ya majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) picha walizomwonyesha, kupeleka katika vyombo vya habari kuonyesha watu walivyochoma milima ya Uluguru, kukata miti na kusababisha mvua kuacha kunyesha.

Kuhusu maji, aliagiza DAWASA kuongeza upatikanaji wa maji mkoani Dar es Salaam na kuhakikisha maji hayo yanawafikia wote bila upendeleo. Pia aliagiza kutekelezwa kwa mpango unaolenga kuwafikia wananchi wote maji safi na salama ifikapo mwaka 2030.

Katika kufanya hivyo, alisema DAWASA, pamoja na mambo mengine, ijitahidi kuchimba visima na kuangalia njia zote ili maji yapatikane pamoja na kudhibiti upotevu wa maji.

"Leo (jana) tumekabidhi mitambo ya uchimbaji visima na mabwawa. Ni matumaini yangu kuwa Wizara ya Maji itasimamia jambo hili na DAWASA ifanye kazi kwa weledi ili kutimiza ile kauli ya kumtua ndoo mama kichwani," alisema.

Alisema wamekabidhi vifaa vya kufanya utafiti katika maeneo yenye maji, hivyo ni muhimu miundombinu ilindwe na kutumika kama ilivyokusudiwa.

"Mitambo na vifaa hivi vitunzwe. Itachekesha kuona mitambo hii muda mfupi tunapata taarifa kuwa imeanza kuharibika. Naomba mtambue hii mitambo imegharimu Sh. bilioni 35 ambazo zingeweza kuelekezwa sehemu nyingine na kufanya mambo mengine makubwa," alisisitiza na kubainisha kuwa iwapo itatumiwa vizuri, itafanya kazi kubwa kwa taifa.

Rais alikumbushia miradi ya maji iliyokuwa ikitekelezwa awali ukiwamo wa visima 10 kila mkoa ambapo zilitumika fedha nyingi lakini maji hayakutoka.

"Asilimia 20 ya mradi ule ulikuja na matokeo chanya lakini sehemu iliyobakia fedha ilipotea na maji hayakupatikana. Unakwenda mahali watu wameweka miundombinu ya kusambaza maji lakini chanzo cha maji hakuna. Maeneo mengine chanzo cha maji kipo lakini hakitoi maji" alisema.

## HABARI KITAIFA

## Shaka: Watanzania watampa Samia tuzo ya heshima na iliyotukuka 2025

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, amesema Watanzania watampa Rais Samia Suluhu Hassan mwaka 2025 tuzo ya heshima na iliyotukuka kutokana na kazi nzuri anayoifanya kuwaletea maendeleo.

Amesema Rais Samia ameonyesha uungwana wa hali ya juu kwa kuendelea kuchapa kazi yenye tija na kuleta matokeo mazuri ikiwamo kutekeleza miradi ya maji yenye lengo la kupunguza na kuondoa tatizo la upatikanaji wake katika maeneo mbalimbali nchini.

Shaka aliyasema hayo jana wakati akizindua mradi wa maji wa Kimbiji ulioko Kigamboni, Dar es Salaam, na kukabidhi mitambo ya kutafuta na kuchimba visima virefu vya maji pomoja na kukabidhi eneo la uchimbaji bwawa la Kidunda kwa mkandarasi atakayetekeleza mradi huo.

“Kwa heshima unayoileta, Watanzania watakupa tuzo iliyotukuka na ya heshima mwaka 2025. Mheshimiwa Rais Samia hongera sana kwa mzigo huu unaochapa,” alisema.

Yuko mshairi alisema na yuko mshairi alitunga tungo ‘ada ya mja ni kunena’ akimaanisha kwamba kawaida ya binadamu ni kusema ‘muungwana ni vitendo’ na kila aliye muungwana atatenda. Mheshimiwa Rais wewe ni muungwana wa taifa hongera sana.

“Akamalizia (mshairi) kusema tenda watu wataona majigambo weka kando. Mheshimiwa Rais unatenda, huna zogo, huna mbwembwe. Unawaletea maendeleo wananchi. Vijana wa mjini wanasema unakimbiza kimya kimya,” alisema.

Shaka alisema pamoja na ukame uliopo sasa ambao umesababisha upungufu wa maji katika maeneo mbalimbali, serikali inafanya kazi nzuri na kwamba Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuanzia kamati za siasa za wilaya, mikoa, sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) na wajumbe wa NEC, wametembelea na kujiridhisha kuna miradi ya maji 1,194, hivyo nchi nzima inaguswa na utekelezaji huo.

## NHC kuwakutanisha wadau 1,000 uzinduzi sera ya ubia

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limesema uzinduzi wa sera ya ubia ya shirika hilo unaotarajia kukutanisha wadau zaidi ya 1,000 wa ndani na nje ya nchi, utaongeza makazi, ajira na mzunguko wa fedha nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Meneja wa Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya alisema uzinduzi wa sera hiyo unatarajiwa kufanyika Novemba 16 mwaka huu jijini.

“Hapo awali tulitenga maeneo 60 tu yenye viwanja na majengo yanayohitaji kuendelezwa lakini tumeamua kuongeza maeneo zaidi ili yaendelezwe.

“Ili kutoa muda wa kuchambua majengo na kuidhinisha maeneo haya mapya yatakayotangazwa wakati wa mkutano huu, shirika limeamua uzinduzi huu kufanyika Novemba 16 mwaka huu,” alisema.

Saguya alisema mgeni rasmi katika uzinduzi huo anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa na mabalozi 20 wanaowakilisha nchi zao nchini, taasisi za kimataifa 10, mawaziri na mahakama wanatarajiwa kushiriki.

Alisema baada ya kutangaza na kutuma mialiko kuomba wawekezaji waunge mkono maono ya shirika kupitia sera hiyo ya ubia, wamejitokeza watu zaidi 1,000.

“Tumeona viwanja 60 havitoshi tukidhi mahitaji ili kujenga majengo makubwa ya biashara na uwekezaji, tumeona tuongeze muda ili tuchambue majengo na viwanja yaliyopitwa na wakati wa kuyanadi, tuna vitabu viwili, cha sera na kingine cha miradi 60 na mingine iliyoongezwa,” alisema.

Meneja huyoa alisema sera hiyo ilianzishwa na shirika mwaka 1993 na kufanyiwa maboresho kadhaa na ya mwisho yamefanyika mwaka huu ili kuondoa vikwazo vilivyojitokeza awali.



Kijana aliyejitosa na kuokoa abiria kwenye ajali ya ndege ya shirika la Precision Air, Majaliwa Jackson, akitambulishwa Bungeni jijini Dodoma jana, alipofika hapo kwa mwaliko wa wabunge. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ajali magari 7 ilivyokatisha maisha ya mwalimu na kumjeruhi mume wake

**Na Beatrice Shayo**

MWALIMU wa Shule ya Sekondari ya Kisanga, Sarah Shirima, amefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa akiwamo mume wa marehemu, baada ya lori kufeli breki na kugonga magari saba katika barabara ya Wazo mkoani Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Mtatiro Kitinkwi, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana saa 1:25 asubuhi na kulitaja lori hilo kuwa ni lenye namba za usajili T 303 ABV aina ya Scania likiwa na tela lenye namba T 577 ASW.

Alisema lori hilo lililokuwa limebeba shehena ya saruji, wakati wa tukio lilikuwa likishuka kilima likitokea kiwanda cha Saruji cha Wazo kwenda Tegeta Kibaoni ndipo lilipofeli breki.

“Hili lori wakati linatoka kiwandani kuelekea Tegeta Kibaoni, lilipofika eneo hilo, lilifeli breki wakati huo magari yanayotokea Wazo kwenda Tegeta Kibaoni yalisimamishwa.

“Na wakati huo, yale yanayotoka Tegeta Kibaoni kwenda Wazo yalikuwa yameruhusiwa, hivyo kusababisha kugonga magari mengine saba,” alisema.

Kamanda Kitinkwi alisema Shirima alifariki dunia wakati akiendelea na matibabu Hospitali za Kitengule na Rabininsia. Aliyataja magari mengine ni T 309 DQC aina ya Toyota IST rangi ya Silver ambalo dereva wake ni Pantaleo Gwinewe (45) ambaye ni mfanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), mkazi wa Mapinga aliyekuwa na mke wake ambaye amefariki dunia.

Majeruhi mwingine, kwa mujibu wa Kitinkwi ni Gilbert Mark (28) ambaye ni mfanyakazi wa Kiwanda cha Saruji Wazo aliyekuwa akiendesha gari namba T 447 DWL aina ya Toyota IST ambaye alipata michubuko ya mikono.

Shuhuda wa ajali hiyo, Godfrey Jackson, alisema wakati ajali hiyo inatokea walisikia sauti ya watu wawili wakiwa wanalia na damu zinamwagika. Alisema jitihada za kuwaondoa kwenye gari lao aina ya Toyota IST zilifanyika kwa kuvunja gari hilo kwa nyundo.

Pia alisema barabara hiyo ya Wazo ni nyembamba na inapotokea ajali hushindwa kwenda upande wa pili wa barabara.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Mnada wa hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | 1. NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA<br>2. NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.1123 KITALU 'L' HATI NAMBA 85726-MBAGALA<br>3. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO-CHAMAZI DOVYA | AHMAD KASSIM OMARY | 1. KIBAMBA<br>2 .MBAGALA<br>3. CHAMAZI DOVYA | 28/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

21714552

# Wavuvi wanavyouhusisha uhaba wa samaki na dhambi

## ●Kinamama wachuuzi walia ugumu wa maisha
## ●Mapato ya wavuvi yatajwa kushuka maradufu

**Na Mary Geofrey**

NI majira ya mchana, katika Soko la Samaki Feri mkoani Mtwara, linaonekana kundi la kinamama wachuuzi wa samaki waliokaa kwa makundi, wakisubiri kitoweo cha samaki kutoka kwa wavuvi.

Kinamama hao, wengi wao wakiwa wamejitanda kwa khanga kichwani, mikononi wameshikilia mabeseni na ndoo za kubebea samaki, tayari kupokea bidhaa kutoka Bahari ya Hindi.

Hata hivyo, kwa mwonekano kundi hilo la wanawake linaonekana dhahiri kutokuwa na matumaini na kile linachokisubiri.

Tatizo nini? Nipashe inasogea eneo la soko na baada ya salamu, wachuuzi wanatoa mrejesho wenye ufafanuzi kwamba kwa sasa kumeshuhudiwa uhaba mkubwa wa samaki katika soko hilo.

"Kama unavyotuona hapa, sasa hivi ni saa sita mchana, hakuna dalili ya kupata samaki, wameadimika lakini pia bei yake ni ghali," analalama Husna Rashid, mkazi wa mjini Mtwara.

Anasema alifika eneo hilo majira ya saa tatu asubuhi akiwa na matarajio ya kununua samaki wa Sh. 40,000 ili kuwakaanga na kuuza mtaani kwake anakotumia mtindo wa kuwapanga kwa mafungu.

"Tangu nimekuja hapa, saa tatu zimepita, zimekuja boti mbili tu na wavuvi, samaki walioletwa wachache na bei yao nayo ni kubwa, wamewauza kwa Sh. 70,000, nimeshindwa kumudu gharama, ninaendelea kusubiri nione kama boti zingine zikija nitapata samaki," anafafanua.

Husna, mama wa watoto watatu anayeweka wazi mumewe hana ajira ya kudumu, anatamba kuwa na uzoefu wa mulongo mmoja katika biashara hiyo, akikiri kwamba sasa hali ni ngumu kutokana na uhaba wa samaki kwenye soko lao.

"Ninalisha familia, ninasomesha watoto na mume anapata huduma za msingi anazotakiwa kupata, kipato chake siyo cha kueleweka, siku akipata akaleta, inakuwa sawa, siku anazokuwa hana tunategemea hii biashara," anasema.

Husna anaamini kuadimika kwa samaki kumetokana na alichosikia ni kuongezeka kwa kina cha bahari na samaki kukimbilia mbali, akibainisha samaki wamekuwa wakipatikana kwa shida kwa miaka mitatu sasa.

"Kila siku bora ya jana! Tunaiomba serikali itusaidie kwa sababu biashara hii tunaitegemea kwa ajili ya kuendesha familia zetu, itusaidie wavuvi wawe na boti za kisasa kufika kwenye kina kirefu," anashauri.



Wachuuzi wakiwa kwenye mnada wa Soko la Samaki Feri mkoani Mtwara wiki iliyopita. **PICHA: MARY GEOFREY**

Fatma Namngumi, mama wa watoto sita na mkazi wa mjini Mtwara, anaungana na Husna kulalamika uhaba wa samaki unaochangia biashara ya samaki kuwa ngumu kwao tangu mwaka 2019.

Hata hivyo, tofauti na mtangulizi wake (Husna), Fatma anaamini kuadimika kwa samaki kwenye eneo lao kumesababishwa na kuchafuka kwa bahari.

"Kila siku wavivu wanalalamika bahari imechafuka, wamekosa samaki. Tangu tumekuja hapa sokoni saa nne asubuhi sijaona dalili ya samaki. Ina maana leo biashara hapa hamna. Hata ukiwapata, bei ya kununulia itakuwa kubwa. Je, nitauzaje nipate faida ya kulisha familia?" Fatma anahoji.

Mchuuzi huyo mwenye uzoefu wa miaka 15 katika biashara hiyo, anabainisha imemwezesha kujenga nyumba, kusomesha wanawe na hata kuweka kwenye vikundi vya kuweka akiba na kukopa (Vicoba) mtaani kwake.

"Kwa kweli biashara inalipa, lakini kwa sasa hailipi tena kwa sababu samaki hamna, bei imeongezeka sana. Tunachokipata ni kwa ajili ya kula na familia tu, huwezi kuweka akiba wala kufanya mambo ya maendeleo," analalamika.

Kuluthumu Mohamed, mchuuzi mwingine aliyekutwa na Nipashe kwenye soko hilo, anasema awali alikuwa ananunua samaki kwa Sh. 30,000 na kujaza beseni kubwa la lita 10, akiuza anapata faida ya Sh. 30,000 hadi 40,000 kutegemeana na anachokiita hali ya msimu.

"Lakini sasa anasema hali imebadilika, samaki tunaonunua kwa Sh. 50,000 tunapata faida ya Sh. 10,000 hadi 15,000 kwa siku na wakati mwingine hawauziki.

"Unakuta una wateja ambao wanataka samaki wa mafungu, kama hivi leo tangu nimekuja hapa ninakutana na samaki wakubwa mmoja anauzwa Sh. 5,000 hadi 7,000 ninanunua wangapi ili niuze na kupata faida?" anahoji.

Kuluthumu anasema kutokana hali iliyopo sasa kiuchumi, njia mbadala kwake ni kuchukua samaki wakubwa wachache kwa gharama ya Sh. 20,000, anawakata vipande na kuwakaanga, kisha kipande kimoja anakiuza kwa Sh. 3,000 ili walau arejeshe mtaji wake na kulinda wateja wake wasipotee.

"Wateja wana tabia ya kuhama wakiona kila siku huna samaki, wanakosa imani na kuanza kwenda kununua kwingine. Kwa hiyo, ukimwambia leo nina hawa hata kama hajawapenda atanunua tu," anasema.

Mchuuzi mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Mama Ashura, anaungana na wachuzi wenzake 'kulia'na hali ngumu ya upatikanaji wa samaki kwenye eneo lao.

Tofauti na watangulizi wake, Mama Ashura anajishughulisha na kukaanga samaki wa wafanyabishara kwenye eneo la Feri, akifafanua biashara kwake imekuwa ngumu kwa kutokana na kupungua kwa wateja.

"Kwa kuwa samaki wamepanda bei kutokana na kuadimika baharini, wafanyabiashara wengi sasa wanawauza wakiwa wabichi au waliobanikwa ili kuendelea kupunguza gharama za kukaanga.

"Gharama za kukaanga samaki katika soko hili ni kuanzia Sh. 3,000, inategemea na wingi wa samaki hasa kwa kuzingatia kuwa mafuta nayo yamepanda bei," Mama Ashura anawasilisha kilio chao.

Yassin Jumanne, anayejishughulisha na kusafisha na kukata kata samaki katika eneo hilo la Soko la Feri, anaamini samaki wameadimika kutokana na mabadiliko ya hali ya bahari.

Anasema gharama ya kukwangua samaki, kuwaosha na kuwakata ni kuanzia 1,000 kulingana na idadi ya samaki, akibainisha kuwa kwa siku alikuwa na uhakika wa kuingiza Sh. 60,000 lakini sasa anaambulia Sh. 15,000 hadi 20,000 kwa siku.

**ITAENDELEA KESHO**



Mfaume Mangoda, mfanyabiashara wa samaki akinadi bidhaa zake kwenye Soko la Feri mkoani Mtwara wiki iliyopita.

## Ukame ulivyoathiri kilimo cha tumbaku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa tumbaku katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameingiwa na hofu ya kukosa mavuno ya kutosha msimu huu baada ya miche ya zao hilo kunyauka kutokana na ukame.

Wakizungumza juzi baada ya kutembelewa na Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Hamisi Majogolo katika vitalu vyao vilivyonyauka, wakulima hao walibainisha kukosa matumaini na zao hilo kwa msimu huu.

Hamisi Bunzali, mkulima kutoka Kata ya Ulowa, alisema miche ya tumbaku imekauka kutokana na ukosefu wa maji unaosababishwa na ukame uliokithiri ambao umechangia maji kukauka kwenye mabwawa waliyoyachimba kwa ajili ya umwagiliaji wa vitalu vya miche.

Alisema kwa msimu huu uzalishaji unatarajiwa kupungua kutokana na wakulima wengi kutokuwa na mbegu za zao hilo kwa kuwa mbegu zilizopo zimekauka kutokana tatizo la ukame na wengi wao watapata hasara kutokana na mikopo waliyopewa na kampuni na taasisi za kifedha.

Samora Mayunga, mkulima kutoka Kijiji cha Kangeme, aliziomba kampuni zinazohusika na ununuzi wa zao hilo kuwasaidia kutatua tatizo la upatikanaji wa maji ili kunusuru miche iliyobakia.

"Tungekuwa na mabwawa makubwa ya maji, tusingepata hasara ya mbegu ambazo tumezitunza kwa gharama kubwa. Zao hili linatumia gharama kubwa kwenye maandalizi hadi kuvuna na tusipoangalia hatutafikia lengo la makisio," alitahadharisha.

Meneja wa Kampuni ya Mkwawa inayojishughulisha na ununuzi wa tumbaku, Alawi Kain alisema kuwa ili kukabiliana na ukame huo wameamua kupeleka maji kwa wakulima kwa kutumia magari makubwa ili kunusuru miche ambayo ilikuwa imeanza kunyauka."Sisi tumeamua kuwapelekea maji wakulima wetu wa tumbaku bure kupitia magari ya maji ili kuwawezesha kukabiliana na tatizo la ukame na zoezi hili litasimama pale mvua ikapoanza kunyesha," alisema Kain.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu ch Ushirika Kahama (KACU) Hamisi Majogolo, aliiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuchukua hatua za haraka kwa kuchimba mabwawa makubwa ya maji ili kuwawezesha wakulima kutunza miche yao katika mazingira salama.

# Samia aagiza 28,000 waliokosa mikopo wapokewe vyuo vikuu

**Na Richard Makore,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza wanafunzi wote 28,000 wa elimu ya juu wenye sifa za kupewa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) lakini wameikosa, wapokewe vyuoni na kuanza masomo.

Kauli hiyo ya serikali ilitolewa bungeni jijini hapa jana na Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa alipotoa hoja ya kuahirisha Bunge baada ya kumaliza shughuli zake za mkutano wa tisa.

Majaliwa alisema Rais Samia ameagiza wanafunzi hao wapokewe vyuoni wakati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akiendelea kufanya ukaguzi maalum kwenye bodi hiyo.

Katika mkutano wa tisa wa Bunge uliomalizika jana, hoja ya wanafunzi 40,000 wa elimu ya juu kukosa mikopo mwaka huu ilitolewa bungeni na Mbunge wa Biharamulo, Ezra Chewelesa.

HESLB kwa mwaka wa masomo 2022/23 ilitengewa Sh. bilioni 570 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kiasi ambacho hakikutosha kwa wahitaji wenye, hivyo wakakopeshwa wanafunzi 42,000.

**HOFU YA NJAA**

Akizungumza bungeni jana, Majaliwa pia aliwataka wananchi kutunza chakula walichonacho badala ya kukifanyia matumizi yasiyokuwa ya lazima.

Alisema kutokana na kuwapo upungufu wa chakula kwa baadhi ya wilaya nchini, serikali imepeleka mahindi ambayo yatauzwa kwa bei ya chini ili kukabiliana na tatizo hilo.

Katika mkutano huo, Bunge lilipitisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24.

Wabunge walipata fursa ya kujadili mpango huo pamoja na mwongozo kwa siku nne na kuhitishwa na mtoaji hoja ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

Serikali inatarajia kutumia Sh. trilioni 43 kwa mwaka ujao wa fedha, huku vipaumbele vikiwa ni kuendeleza miradi yote mikubwa inayotekelezwa nchini.

Bunge liliahirishwa jana hadi Januari 31 mwakani.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, akikabidhi cheti cha shukrani kwa Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, kilichotolewa na Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), kwa kuunga mkono chemba hiyo, katika hafla iliyofanyika mkoani humo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mwinyi aitupa hoja ya ACT uteuzi Mkurugenzi wa NEC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya Chama cha ACT Wazalendo kupinga uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi katika Tume ya Uchaguzi (ZEC), Thabit Idarous Faina uliofanywa juzi na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, kiongozi huyo jana alimwapisha mteule wake huyo kushika wadhifa huo.

Dk. Mwinyi alimwapisha mkurugenzi huyo pamoja na viongozi wingine aliowateua wakiwamo makatibu wakuu kwa baadhi ya taasisi katika serikali yake.

Hafla hiyo ilifanyika Ikulu Zanzibar ambapo viongozi hao baada ya kiapo, walimshukuru Dk. Mwinyi kwa kuwaamini na kuwapa nafasi na kuahidi kutekeleza majukumu yao.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa ZEC, Faina, alisema vyama vyote vya siasa 19 vilivyosajiliwa Tanzania ni wadau wake na watashirikiana katika kufanya kazi.

Alisema bila vyama vya siasa, hakutakuwa na uchaguzi, hivyo ni vyema kufanya kazi kwa ushirikiano na vyama hivyo.

"Watambue kwamba kama mkurugenzi nipo pale kwa ajili ya kuteleleza sheria ambazo zinaiongoza ZEC, hivyo katika utekelezaji wa majukumu yangu nitahakikisha ninafanya kazi kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na sitokwenda kinyume katika hilo," aliahidi.

Awali chama cha ACT Wazalendo katika taarifa iliyotolewa na Kaimu Naibu Katibu Mkuu, Salum Bimani, kilibainisha kuwa kimepokea kwa masikitiko makubwa uteuzi wa mkurugenzi huyo kwa sababu alishawahi kushika wadhifa huo katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ambao ulileta shida kubwa kitaifa.

Bimani alisema kuwa katika uchaguzi huo, tume hiyo chini ya mkurugenzi huyo iliwaengua wagombea wa chama hicho 16 na kumhusisha na kitendo hicho kwa kutumia vibaya nafasi yake.

Bimani alimtaka Rais Dk. Mwinyi kutengua uteuzi wa mkurugenzi huyo ili kujenga imani kuwa amedhamiria kuleta maridhiano na utengamano wa kweli hasa baada ya kazi kubwa iliyofanywa na kikosi kazi alichokituеua kwa lengo la kujenga mustakabali mpya wa kidemokrasia.

Wengine walioapisha katika hafla hiyo ni Dk. Islam Seif Salum kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Maryam Juma Sadala kuwa Katibu Mkuu (Kazi na Uwezeshaji katika Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na Abeida Rashid Abdallah kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Pia alimwapisha Khamis Abdulla Said kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Saleh Juma Mussa kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Ikulu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga maandalizi ya makundi yaanze sasa

**WAKATI** akiahirisha mkutano wa tisa wa Bunge jijini Dodoma jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alizipongeza klabu za Simba na Yanga kwa kutinga hatua ya makundi katika mashindano ya ngazi ya klabu barani Afrika.

Majaliwa alisema serikali inazipongeza timu hizo kwa kufanikiwa kutinga hatua ya makundi katika Klabu Bingwa barani Afrika na Kombe la Shirikisho kwa pamoja, jambo ambalo linazidi kuitangaza nchi kimataifa.

"Nazipongeza klabu zetu kwa kufanya vizuri katika mashindano ya Afrika na kutinga hatua ya makundi. Kwa Simba wao wametinga hatua ya makundi katika Ligi ya Mabingwa Barani Afrika na Yanga kombe la Shirikisho," alisema Waziri Mkuu.

Aliongeza; "Kipekee naipongeza klabu ya Yanga kwa kuibuka na ushindi wa kihistoria dhidi ya timu ya Afrika Kaskazini na kuingia kwa kishindo hatua ya makundi katika Kombe la Shirikisho Barani Afrika."

Pamoja na pongezi za Waziri Mkuu, Nipashe tunapenda kuzikumbusha Simba na Yanga kwamba, maandalizi ya kuelekea kwenye hatua ya makundi yanatakiwa kuanza sasa.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba, timu zote ambazo zimefuzu kwenye hatua hiyo kabla ya makundi na ratiba zake kupangwa ni tishio na zenye historia kubwa katika mashindano hayo.

Hivyo sisi tukiwa kama wadau wakubwa wa mchezo wa soka, tunaona kwamba, kwa klabu zetu za Simba na Yanga zinatakiwa kutumia vizuri muda walionao kwa sasa wakati wakiendelea na Ligi Kuu kujipanga kwa ajili ya hatua hiyo.

Kuingia kwenye hatua ya makundi ni jambo la sifa kwa timu zote, lakini ukweli ni kwamba, timu wanazokwenda kukutana nazo kwenye hatua hiyo sio rahisi hata kidogo, hivyo wanahitaji muda zaidi wa kuviboresha vikosi vyao.

Katika hatua ya awali ya kufuzu kwa hatua hiyo, timu hizo zitakuwa zimeona mapungufu yao katika maeneo mbalimbali, hivyo zinatakiwa kukaa na kutafakari namna gani wanaweza kuyafanyia kazi hayo kabla ya kuingia kwenye mtanange huo wa makundi.

Ikumbukwe kuwa hatua ya makundi, kila kundi kunakuwa na timu nne, hivyo hivyo mbili za juu ndio zinasonga hatua ya robo fainali, nusu fainali na baadae fainali, hivyo kutakuwa na ushindani wa hali ya juu.

Kutokana na ukweli kwamba, Simba na Yanga hazijafikia hatua ya juu zaidi ya mashindano hayo ya ngazi ya Klabu kwa Afrika kwa muda wa miaka mingi, hivyo zitaingia kama wageni wasiokuwa na uzoefu mkubwa.

Lakini tunaamini kama watajipanga na kujifua vya kutosha wanaweza kutoa ushindani mkubwa na hatimaye kufika hatua ya juu zaidi na hatimaye kubeba mataji hayo ambayo wanayawania.

Kiwango walichoonesha kwenye hatua ya awali ya kuwania kufuzu hatua ya makundi wanaweza kukiboresha zaidi na wanaweza kufanya vyema zaidi kwenye makundi, kwani uwezo huo wanao.

Mabenchi ya ufundi ya Simba na Yanga kwa namna yoyote tunaamini yatafanyia kazi mapungufu yote waliyoyaona wakati wa hatua ya awali na sasa watakuwa wanakuna kichwa namna ya kuyafanyia kazi.

Tunaimani kwamba, hata timu nyingine zilizofuzu hatua hiyo kutoka mataifa mengine zitakuwa na hofu ya kukutana na Simba na Yanga hasa baada ya kushuhudia viwango walivyoonesha wakati wa hatua ya kufuzu.

Hivyo wachezaji wa Simba na Yanga wanapaswa kutumia vizuri maagizo na maelekezo ya mabenchi yao ya ufundi kwa ajili ya kufanya vizuri kwenye hatua hiyo, kwani hiyo pia ni fursa nzuri kwao.

Kwa kuwa hatua ya makundi itashuhudia timu zote kwenye kundi moja zitacheza nyumbani na ugenini, hiyo itakuwa fursa nzuri kwa wachezaji kujiuza kimataifa kwa kuonesha viwango vyao vya juu kabisa.

Tunaamini Simba na Yanga zina nafasi kubwa ya kufanya vizuri zaidi kwenye hatua ya makundi kama tu maandalizi yao yataanza sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba, Yanga ziboreshe vikosi vyao kwa michuano ya kimataifa

Na Adam Fungamwango

**JUMATANO** iliyopita Tanzania iliingia kwenye historia ya aina yake baada ya klabu mbili kongwe nchini, Simba na Yanga zote kuingia kwenye hatua za makundi ya michuano ya kimataifa.

Hii ni rekodi ya aina yake kwani mara nyingi timu hizi zimekuwa zikibadilishana tu, Yanga ikitwaa ubingwa Simba inabaki na inakuwa kinyume chake kama Simba ikitwaa ubingwa.

Ni msimu mmoja tu ambao timu za Tanzania zilikuwa kwenye hatua za makundi pamoja msimu wa 2020/21 wakati Namungo ilipotinga hatua hiyo kwenye Kombe la Shirikisho, na Simba ikawa kwenye hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika.

Msimu huu tunakwenda kuziona timu kubwa zenye mashabiki wengi nchini zote zikiwa kwenye hatua za makundi, Simba kama kawaida ikiwa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na Yanga ikitinga Kombe la Shirikisho.

Simba ilitinga hatua hiyo baada ya kuifunga Primeiro de Agosto ya Angola na Jumatano iliyopita Yanga ilifanikiwa kutinga hatua hiyo kwa kuitoa Club Africain ya Tunisia bao 1-0.

Ni hatua ya kupongezwa kwenye soka la Tanzania kwani imeiweka kwenye mazingira mazuri mwakani kuendelea kuwakilishwa na timu nne bila ya kujali kama zitafanya vema kwenye mechi zao au la.

Hata hivyo, pamoja na kupongeza hatua hiyo, lakini nazitahadharisha timu hizo kuwa pamoja na wanachama na mashabiki zao wanafurahia hali hiyo, lakini wanapokwenda ni pagumu zaidi kuliko walikotoka.

Sizitishi na hizi si zama za kuogopa timu, kwani tumeona matokeo ya ajabu na ya kushangaza, ikiwemo kusukumizwa nje ya michuano ya Kombe la Shirikisho msimu uliopita, RS Berkane ya Morocco, lakini kwa sasa Simba na Yanga zinatakiwa ziboreshe vikosi vyao. Kwa vikosi vilivyonavyo, ni kweli zinaweza kushinda, lakini zitapata tabu sana.

Kwa upande wa Yanga naona kinachotakiwa kurekebishwa ni sehemu ya ulinzi kwani imekuwa na tatizo. Pamoja na kwamba walicheza vema kwenye mechi dhidi ya Club Africain, lakini timu hiyo ilionekana ina wachezaji wazito, wasio na mbio. Kama Yanga ikipata wapinzani wenye wachezaji wepesi na kasi, huwa inakatika na kufanya makosa mengi.

Msingi na nguvu kubwa ya Yanga ipo kwenye viungo, ina wachezaji viungo wa kukaba wenye uwezo wa hali ya juu ambao wanaifanya beki kutulia na kusawazisha makosa madogo madogo tu.

Mbele inatakiwa itafute mbadala wa Fiston Mayele, kwani amekuwa peke yake ndiyo straika hatari mbele bila msaidizi yeyote wa maana. Michuano ni mirefu na Yanga ina mashindano mengi, Ligi Kuu na Kombe la FA.

Simba ukiitazama kiufundi ina matatizo mengi kuliko Yanga. Haina kiungo wa kukaba wa kiwango cha michuano ya Ligi ya Mabingwa. Inatakiwa isajili kiungo wa uhakika na hawa waliopo sasa Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute wawe wanamsaidia. Ikienda huko na kiungo kama Jonas Mkude kwa kiwango chake cha sasa ambacho anaweza asipate namba hata Azam FC, basi wamekwisha.

Simba inatakiwa ipate kiungo mshambuliaji wa kumsaidia Clatous Chama ambaye kama asipokuwepo ni kama tu timu yenyewe haipo. Timu yote ya Simba akikosekana yeye hakuna tena ubunifu, hayo ni makosa makubwa kwa timu inayocheza kimataifa.

Inatakiwa pia kusajili straika mmoja mkubwa mwenye uwezo wa hali ya juu ili kusaidiana na Moses Phiri.

Simba kwa sasa inakosa straika mwenye asili kama Chris Mugalu akiwa kwenye kiwango chake ambaye anaweza kumiliki mipira akiwa na mabeki wa timu pinzani. Mbali na kumiliki, awe pia na uwezo wa kufunga mabao. Inatakiwa pia ipate beki wa pembeni mwenye uwezo wa kucheza namba zote mbili ili kuwafanya wanachama na mashabiki wa Simba akiumia Shomari Kapombe au Mohamed Hussein 'Tshabalala' basi hawana amani.

Kama timu hizo zikifanikiwa kuziba mapengo hayo zinaweza kabisa kushangaza Afrika na Tanzania ikang'aa zaidi.

HABARI KITAIFA

# Kima cha chini mishahara ya sekta binafsi kutangazwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa mwezi huu inatarajia kutangaza kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa sekta binafsi baada ya kukamilisha kazi ya upangaji.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, alitoa ahadi hiyo bungeni jijini hapa jana alipojibu swali la Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo.

Mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali kutoa muongozo wa upandishaji mishahara kwa wafanyakazi wa sekta binafsi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Katambi alisema mshahara katika sekta binafsi unapanda baada ya Bodi ya Kima cha Chini cha Mishahara katika sekta hiyo inayoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300 kufanya utafiti na kupanga viwango vya mishahara katika sekta binafsi.

Alibainisha kuwa bodi hiyo tayari imekamilisha kazi ya kupanga kima cha chini kipya na kumshauri waziri mwenye dhamana na masuala ya kazi ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kutangaza kima cha chini hicho.

"Serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha kazi ya upangaji na itatangaza kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa sekta binafsi mwezi huu," alisema.



Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (kushoto), akikabidhi hundi ya 800,000/- kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Misufini B, Asha Usi, kwa ajili ya kusaidia kuweka umeme, shuleni hapo mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbunge akabidhi madawati 500

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood amemaliza kero ya wanafunzi kuketi sakafuni kutokana na upungufu wa madawati katika shule za msingi zilizopo katika manispaa hiyo baada ya kutoa jumla ya madawati 500 yenye thamani ya Sh. milioni 45 pamoja na fedha kwa ajili ya kuingiza umeme kwenye shule hizo.

Shule zilizokuwa na kero hiyo na kupatiwa madawati hayo ni pamoja na shule za msingi Kiwanja cha Ndege, Misufini B, Sabasaba A na B pamoja na Mwembesongo.

Akizungumza wakati akikabidhi madawati hayo kwenye shule hizo kwa nyakati tofauti juzi, Abood alisema lengo lake ni kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuiinua sekta ya elimu hapa nchini.

Abood alisema Rais Samia amekuwa kifanya kazi kubwa kwenye sekta mbalimbali ikiwamo ya elimu, hivyo naye ameona umuhimu wa kuungana naye kuhakikisha wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi wanaondokana na shida ya upungufu wa madawati ili wapate elimu bora.

"Mimi kama Mbunge wa Morogoro Mjini, kwanza kabisa ninamshukuru Rais Samia kwa kutuletea fedha nyingi katika sekta ya elimu ambazo zimeondoa kero ya upungufu wa madarasa na mimi nimeona nimuunge mkono kwa kuchangia madawati kwa watoto wetu wa shule za msingi," alisema.

Mbunge huyo alisema yupo tayari kuendelea kutoa misaada katika sekta ya elimu katika shule za manispaa hiyo ili kuunga mkono jitihada za Rais Samia ambaye amekuwa akifanya kazi kubwa kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu katika mazingira bora.

Baada ya kupokea madawati hayo pamoja na hundi ya Sh. 800,000 kwa ajili ya kuweka umeme, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Misufini B, Asha Usi, alimshukuru Mbunge Abood kwa msaada huo ambao umetolewa kwa wakati kutokana na kuwapo kwa upungufu wa madawati na tatizo la umeme.

Alisema kutokana na kuwapo upungufu wa madawati, wanafunzi wa shule hiyo walikuwa wakilazimika kuketi sakafuni huku wakiandika kwa shida na wengine kulalamikia maumivu mgongo na baadhi yao kushindwa kufanya vizuri katika masomo yao.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hizo zilizopatiwa msaada huo wa madawati, kwa nyakati tofauti wameshukuru Mbunge Abood kwa madawati hayo na kuahidi kuyatunza vizuri ili yaendelee kudumu.

# Uchunguzi mikopo asilimia 10 waanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UCHUNGUZI wa utoaji mikopo ya asilimia 10 kwenye halmashauri nchini umeanza kwa kuhusisha vyombo mbalimbali kutokana na kudaiwa kutolewa kwa wasio walengwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Angellah Kairuki alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa wakati wa kikao cha maofisa maendeleo ya jamii.

Alisema uchunguzi huo utaangalia tangu kuanza utoaji wa mikopo hiyo na yeyote atabainika kufanya ubadhirifu kwenye mikopo hiyo, atachukuliwa hatua bila kujali nafasi yake.

"Kwa sasa kuna kesi nyingi za watu waliopewa mikopo hiyo ambao si walengwa, kuanzia Januari (mwakani) vumbi litatimka, vyombo vimeingia kazini kupitia mikopo yote kuanzia mpango huu ulipoanza na hatutakuwa na hiyana na yeyote. Kama ni diwani hatutaangalia nafasi ya mtu kwenye jambo hili," alitahadharisha.

Alisema wanaopitia utoaji mikopo hiyo si Ofisi ya Rais - TAMISEMI pekee, bali vyombo vyote vya kiuchunguzi.

"Mtaona vumbi litakalofuata, kama ulikuwa na 'madudu' yako, ni vyema ukajisalimisha mapema na kuleta mpango wa marejesho, kama ulikuwa unakula nao, wewe ingia 'inbox' kabisa wataje au waliokushinikiza, pia vilivyokushinikiza tuvijue," alisisitiza.

Aliwataka maofisa hao kuwa makini wanapotoa mikopo ili kujiepusha na utoaji mikopo kwa vikundi hewa na kuwataka kutoa elimu kwa walengwa hao.

"Nendeni mkaangalie aina ya watu mnaowapa mikopo kwani kuna vikundi hewa, ninaomba tusifikishane sehemu ambayo siyo, wengine wanashirikiana na madiwani vinatengenezwa vikundi hewa, fedha inaingia na kikundi kinasambaratika, tunakuja huko sasa msije mkapata matatizo, ninadhani mnafahamu vizuni na msije sema sikuwaambia," alisema.

Kairuki alisema haoni sababu maofisa hao kutumia mikopo hiyo kujineemisha kwa sababu wao hajakatazwa kufanya shughuli zingine za kiuchumi nje ya halmashauri zao.

"Hakikisheni mnasimamia urejeshaji wa mikopo hii na katika mwaka wa fedha 2022/23 tumepanga kukusanywa marejesho ya Sh. bilioni 75," aliagiza.

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainabu Chaula aliwataka maofisa hao kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

# Wilaya ya Ikungi yapewa tani 60 za chakula

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

WAKALA wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) imetoa tani 100 za mahindi sawa na magunia 2,000 kwa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida ambayo yatauzwa kwa wananchi kwa bei nafuu ili kukabiliana na upungufu wa chakula.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Ikungi, Justice Kijazi, akizungumza jana baada ya kukabidhiwa mahindi hayo, alisema yatauzwa kwa Sh. 830 kwa kilo kwa wananchi ambao hawana uwezo wa kununua mahindi kwa bei ya sokoni ambayo ni Sh.1, 200 kwa kilo.

Kijazi alisema mahindi hayo yatasaidia kupunguza upungufu wa chakula kwa wananchi kwa kuwa wilaya katika msimu wa kilimo wa 2021/22 ilivuna mazao ya chakula chini ya kiwango, hivyo kuwa na upungufu wa asilimia 47 ya chakula. "Nawashukuru Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu na mbunge wa Singida Magharibi, Elibariki Kingu, na Wizara ya Kilimo ambao wamepigania hadi kuletwa kwa mahindi hayo," alisema.

Naye Ofisa kutoka NFRA Dodoma, Restuta Josephat, alisema wakala kwa awamu ya kwanza imeleta tani 30 sawa na magunia 600 ya mahindi na tani 70 zilizobaki zitaletwa hivi karibuni.

Josephat aliwaomba wananchi wa wilaya ya Ikungi kujitokeza kwa wingi kufika katika ghala la kijiji cha Ikungi kwa ajili ya kununua mahindi hayo ambayo yatakuwa yakiuzwa kwa bei nafuu.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Wilaya ya Ikungi, Gurisha Msemo, alisema katika kuhakikisha mahindi hayo wanauziwa walengwa wilaya imefanya utambuzi kwa kaya zenye upungufu wa chakula kwa kata zote. "Kila mwananchi aliyetambuliwa atakuja na barua za utambulisho kutoka kwa wenyeviti wa vitongoji na vijiji ili kuepuka wafanyabiashara wasiingilie kununua mahindi hayo," alisema.

Msemo alisema wilaya ya Ikungi katika msimu wa kilimo wa 2021/22 ililenga kuzalisha tani 303,703 za chakula lakini kutokana na hali ya mvua kuwa mbaya, zilizalishwa tani 153,079, hivyo kuwa na upungufu wa asilimia 47 ya matarajio ya mavuno.

Aliongeza mahindi hayo yaliyotolewa yatawatosheleza wananchi katika kipindi cha miezi minne kuanzia Novemba hadi Machi, mwakani na kwamba bado kunahitajika tani 27,782.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Ally Mwanga, alisema hivi sasa kuna mfumuko mkubwa wa bei za vyakula kwenye masoko hivyo kutolewa kwa mahindi hayo kutasaidia sana wananchi ambao hawana uwezo wa kununua mahindi kwa bei ya Sh. 1,200 inayouzwa sokoni.

"Tunaishukuru serikali kwa jinsi inavyowajali wananchi wake na wabunge na tutahakikisha mahindi haya wanauziwa walengwa," alisema. Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ikungi, Stamili Dendego, alisema mahindi hayo yamekuja muda mwafaka hivyo wananchi wajitokeze kuyanunua katika maeneo yaliyowekwa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, aliwatahadharisha wafanyabiashara wasithubutu kuingilia ununuzi wa mahindi hayo kwa kuwarubuni wananchi kwani watakaobainika watachukuliwa hatua kali.



Baadhi ya wageni wakifuatilia mada mbalimbali kwenye maadhimisho ya Siku ya Wahasibu Duniani, yaliyoandaliwa na Chama cha Wanawake Wahasibu Tanzania (TAWCA), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wahasibu wakumbushwa kuzingatia maadili

**Na Joseph Mwendapole**

WAHASIBU na wakaguzi wa hesabu nchini wametakiwa kuweka mbele maslahi ya umma, kuwa waadilifu na kuzingatia maadili na sheria zinazowaongoza kwenye kazi zao za kila siku.

Wito huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), Prof. Sylivia Temu, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wahasibu Duniani.

"Tuzingatie uzalendo na maslahi ya taifa lakini pia nimewaasa tusijifungie kwa sababu dunia imekuwa kama kijiji, hivyo tujipange tuwe na mtazamo mpana ili tuweze kufanyakazi za kimataifa kama Umoja wa Mataifa.

"Nimewaambia wahasibu kwamba tumeshaandika hadithi ya miaka 50 iliyopita sasa tujiulize miaka 50 ijayo tunafanya nini ili tuwe endelevu tusiwe wale wale tu tunatakiwa kwenda sanjari na mabadiliko," alisema.

Pia alisema NBAA imeshaanza kuonyesha mfano kwa kufanya kazi za kihasibu kimataifa ambapo wameanza kutoa ushauri Msumbiji na Malawi na wanatarajia kwenda kwenye mataifa mengine.

Alisema wahasibu na wakaguzi wanapopata kazi za kimataifa wasizikatae kwani zitailetea heshima nchi na wahasibu wa Tanzania watapata sifa kwa umahiri na ubobezi kwenye fani hiyo na pia itawaongezea uchumi.

Prof. Temu aliwataka wahasibu na wakaguzi wapambane kuikuza taaluma yao katika nyanja ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kwenda na kasi ya teknolojia duniani.

"Tukiachwanyuma kiteknolojia nirahisi watu wengine wakafanyakazi ambazo siyo za uadilifu kwa kutumia teknolojia hiyo lakini sisi tukiwa vizuri kweneye teknolojia tutaweza kusimamia vizuri rasilimali fedha," alisema.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumteua kuwa mwenyekiti wa bodi wa kwanza mwanamke wa bodi hiyo kwa miaka 52 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1972.

"Namshukuru kwa kuniamini na muahidi kwamba nitafanya kazi na wenzangu kwa uaminifu mkubwa kuhakikisha fani hii inafanyika kwa uadilifu mkubwa," alisema

Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, CPA Pius Maneno, alisema maadhimisho hayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka na sherehe hizo mwaka huu zinaenda sanjari na maadhimisho ya miaka 50 ya NBAA iliyoanzishwa 1972.

Alisema NBAA imefanya mambo mengi kuongeza idadi ya wahasibu nchini ambao kwa sasa wako zaidi ya 26,000 na imefanya ukaguzi kwenye makampuni 450 kuangalia kama yanafuata matakwa ya sheria.

"NBAA imeongeza idadi ya watahiniwa kwasasa mitihani ambayo inafanyika Novemba au Mei kunakuwa na wanafunzi kama 7,000 wanaofanya mitihani hiyo na tumetoa miongozo mbalimbali," alisema.

Alisema miongoni mwa mafanikio ya NBAA ni nchi mbalimbali kuja kujifunza namna ya kufanya kazi za kihasibu kwani kwa sasa NBAA inamkataba wa miaka mitano na serikali ya Msumbiji kufundisha masuala y uhasibu na fedha kwenye sekta ya umma.

Alisema kwa miaka hiyo 50 NBAA imefanikisha kuwa na majengo yake yenyewe na kuwa na kituo cha Wahasibu Bunju APC na kwamba wamekutana kwenye maadhimisho hayo wahasibu wa zamani na wa sasa kubadilishana mawazo namna ya kuboresha taaluma.

## TAWA yafundwa usimamizi miradi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

NAIBU Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Juma Mkomi ameitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kuongeza jitihada za usimamizi wa miradi ya maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO -19 ili kuleta tija inayokusudiwa na serikali.

Mkomi alisema hayo jana alipofanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na TAWA kupitia fedha za ujenzi za UVIKO-19 katika Pori la Akiba Wamimbiki lililoko katika mikoa ya Morogoro na Pwani.

"Tuongeze jitihada za usimamizi mzuri wa hii miradi ili iweze kuleta tija iliyokusudiwa. Sambamba na hilo hakikisheni mnatenga bajeti miradi hii iwe inafanyiwa matengenezo ya mara kwa mara ili isipoteze ubora wake hususani barabara," alisema.

Kaimu Naibu Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mlage Kabange, alisema kupitia mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO - 19, mamlaka ilipokea Sh. bilioni 12.9.

Kamishna Kabange alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 2.1 zilipelekwa kwenye Pori la Akiba Wamimbiki kwa ajili ya miradi ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 47.2 ambao umegharimu Sh. bilioni 1.3.

Pia alisema Sh. milioni 577 zilipelekwa kwenye ujenzi wa lango la kuingia wageni ambalo linajumuisha kituo cha habari, eneo la kupumzika wageni, eneo la kuuza bidhaa za asili na vinywaji pamoja na nyumba ya askari.

Kabange alisema pia Sh. milioni 152 zimepelekwa kwenye ukarabati wa mabanda ya kupumzika wageni. Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufanikisha upatikanaji wa fedha hizo, ambazo zimeisaidia TAWA kuboresha miundombinu ya utalii katika maeneo inayosimamia.

# Wafanyabiashara wakwepa kutumia EFD

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesema rekodi zake zinaonyesha kuwa kuna wafanyabiashara 347 wa mkoa wa Manyara hawatumii mashine za kielektroniki za ukusanyaji wa mapato (EFD).

Kwa mujibu wa TRA, wanaotumia mfumo huo kwa Manyara ni wafanyabiashara 3,052, ambao baadhi yao wanakabiliwa na kasumba ya kukwepa kutoa stakabadhi kwa wateja wao.

Akizungumzia hali ya ukusanyaji wa mapato mkoani hapa jana, Ofisa Elimu na Huduma kwa Mlipakodi wa TRA Mkoa wa Manyara, Serapio Luanda, alisema walibaini udanganyifu wa wafanyabiashara kutoa stakabadhi baada ya kukagua wafanyabiashara 74.

"Tumewatembelea wafanyabiashara ambao hawana mashine za EFD na tumewahimiza kununua mashine hizo ili wazitumie kukwepa mkono wa sheria watakapokutwa hawana tena mashine hizo.

"Wafanyabiashara 347 wanahitajika kutumia mashine za EFD kwa kuwa tayari biashara zao ziko kwenye kundi la kutumia mashine hizo," alisema.

Kutokana na udanganyifu unaoendelea, Luanda alisema TRA imeanzisha programu maalumu ambayo inatambulika kama mwaka wa EFD ikilenga zaidi kutoa elimu ya kina kwa wafanyabiashara.

Katika kikao kazi maalum, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema wafanyabiashara wanapaswa kujua kwamba kutumia mashine hizo ni takwa la kisheria na si ombi.

"Matumizi yake yalianza mwaka 2010. Sasa wafanyabiashara wanaolazimishwa na sheria kutumia mashine za EFD ni wenye mauzo ya kuanzia Sh. milioni 11. Mfanyabiashara kutotumia EFD ni kosa kisheria na faini ya kutokutoa risiti (stakabadhi) ni Sh. milioni tatu mpaka milioni 4.5

"Na kwa mteja ambaye hadai risiti faini yake inaanzia shilingi 30,000 mpaka milioni 1.5 au kifungo kwa mfanyabiashara au mteja aliyeshindwa kudai risiti," alisema.



Baadhi ya washiriki wa Semina ya Jinsia na Maendeleo (GDSS), iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wakiwa katika vikundi vya kujadili mikakati ya kutokomeza ukatili wa jinsia, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kampeni hamasa elimu kwa wafugaji yaja

**Na Cynthia Mwilolezi,** MONDULI

WILAYA ya Monduli mkoani Arusha, inafikiria kuanzisha kampeni maalum ya hamasa ya elimu, kwa ajili ya kuifungua 'macho' jamii ya kifugaji ya Kimasai, kupeleka watoto wao shuleni hasa wasichana.

Kampeni hiyo itazilenga zaidi koo za kifugaji zilizoko pembezoni mwa wilaya ambazo hazipeleki watoto shuleni kutokana na usiri wa matumizi ya mila na desturi potofu.

Ofisa Elimu Msingi wa Wilaya hiyo, Natang'aduaki Mollel, alidokeza jana kuhusu ujio wa kampeni ya hamasa ya elimu kwa wafugaji, alipokuwa akizungumza na wazazi na walezi katika mahafali ya 40 ya Shule ya Sekondari Moringe.

"Tutapeleka zaidi elimu kwa jamii ya kifugaji, hasa kule pembezoni ambako wanaishi kama wako peponi na hakuna serikali.

Tunadhani iko haja wapelekwe wadau wa asasi za kiraia zinazoshughulika na masuala ya elimu na haki za binadamu ili wakatoe hamasa ili wawe na mwamko wa kupeleka watoto shule kwa wingi na kuachana na mila potofu zinazozorotesha elimu," alisema.

Kwa mujibu wa Mollel, mwamko wa elimu kwa jamii ya wafugaji hususani waishio pembezoni, bado ni tatizo kubwa na linachangiwa viongozi wa mila kuwabana wafugaji wanaoamua kuandikisha watoto kuanza darasa la kwanza.

Katika mahafali hayo, Katibu wa Idara ya Elimu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Loshilu Sambweti, alisema suala la elimu kwa jamii ya wafugaji, bado ni tatizo, kwa kuwa idadi ya wanaoandikishwa ni ndogo, ikilinganishwa watoto wanaobaki kwenda kuchunga mifugo, na wasichana kuozeshwa wakiwa na umri mdogo.

Vilevile, Sambweti alisisitiza kuwa tatizo hilo linachangiwa na kutokuwepo kwa uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa elimu katika jamii hiyo.

"Ukiangalia katika wilaya za Kiteto, Simanjiro, Longido na Monduli, watoto wa kike wanaozeshwa wakiwa wadogo, huku vijana wengi wakikimbilia mjini kutafuta kazi za ulinzi," alisema.

Awali, Mkuu wa Shule hiyo, Lazaro Ndooki, alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika mitihani yake ya kila mwaka, huku akiahidi katika mtihani wa mwaka huu, hakuna mwanafunzi atakayefeli hata mmoja.

## Kanisa lawakumbuka walio katika umaskini

**Na Allan Isack,** ARUMERU

KANISA Katoliki, Jimbo Kuu la Arusha, limeanzisha mradi maalum wa kuwainua kiuchumi watu wenye hali ngumu na wanaotoka katika kaya masikini na kurejesha matumaini ya kujipatia kipato halali katika wilaya ya Arumeru.

Mradi huo unasimamiwa na asasi ya kiraia ya AAIDRO iliyoko chini ya Idara ya Jinsia na Wanawake ya Jimbo hilo.

Akizungumza jana wakati wa kuutambulisha rasmi mradi huo, Padri Faustine Moshi alisema walengwa watakaoanza kunufaika ni wananchi wa kata za Nduruma na Bwawani katika halmashauri ya Arusha.

"Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja na utahusisha makundi rika tofauti. Lengo letu ni kuwawezesha wananchi kijiinua kiuchumi. Kanisa liliguswa na likaona ni vyema kushirikiana na serikali kuwahudumia wananchi katika sekta nyingine zaidi ya ile ya kiroho.

"Utekelezaji wa mradi huu, utagharimu takribani shilingi milioni 230. Tunalenga kuwajengea uwezo watu 200 kupitia vikundi, hivyo ni matumaini yetu, kazi hii itafanywa na Kanisa na watalamu kutoka serikalini kupitia halmashauri," alisema.

Kabla ya uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi aliseam wanashirikiana na Jimbo Kuu la Arusha la Kanisa Katoliki kwa kuwa ni jukumu la serikali kuweka mazingira rafiki, kwa mashirika yanayofanya kazi za kuhudumia jamii kulingana na mpango mkakati wake.

Mratibu wa mradi huo, Irene Moshi, alisema mradi huo utajikita kuwapa mafunzo wakulima ya kufanya kilimo cha kisasa pamoja na kuelekeza nguvu zaidi katika kilimo biashara.

"Kupitia mradi huu, tunategemea kuiwezesha jamii kuwa na uwezo wa kujikomboa kifikra, kujitegemea kiuchumi, kujipatia pato la familia na kuwa jamii huru isiyokuwa na ukatili wa aina yoyote katika masuala ya kijinsia," alisisitiza Moshi.

# Bodi zatwishwa zigo uchimbaji visima

**Anjela Mhando,** SIHA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, imezitwisha mzigo wa ugharamiaji wa miradi ya uchimbaji wa visima virefu vya majisafi, Bodi za Maji za Magadini/Makiwaru na Lawate/Fuka ili kukabiliana na upungufu wa maji, unaowatesa wananchi wake kwa sasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Upendo Mangali, alizitumia wito bodi hizo za maji, wakati akijibu hoja za Madiwani kuhusu tishio la uhaba wa maji linaloathiri shughuli za kiuchumi.

Mangali alikuwa akijibu hoja hizo katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Wilaya hiyo kilichoketi juzi.

"Ni kweli Waheshimiwa Madiwani, kwamba jambo hili linaathiri mambo mengi hasa shughuli za uzalishaji. Nitoe wito kwa bodi zote kutenga fedha katika mapato yao ndani, kwa ajili ya kuchimba visima ili kukabiliana na upungufu wa maji uliopo," aliagiza Mangali.

Alisema uamuzi huo unalenga kuziamsha bodi hizo za maji, kuibua vyanzo vipya vya maji kama kuchimba visima na kuacha kuwa tegemezi wa vyanzo vya mito na maji ya mtiririko ambayo yamepungua vyanzo vingine kukauka kutoka na ukame.

Mkurugenzi huyo, alisema ameshauriana na Meneja wa Wakala wa majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani hapa na wameafikiana wafanye uchunguzi kwenye bodi zote, kwa kutumia wakaguzi wa ndani ili kujua kwa mwezi wanakusanya fedha kiasi gani cha fedha.

Baada ya uchunguzi huo, serikali itaagiza pesa hizo zielekezwe kwenye uchimbaji wa visima.

Diwani wa Sanya Juu, Juma Jani, akizungumzia tatizo hilo, alimshauri Mangali kukumbushia barua aliyoandika kwenda kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, kuomuomba kwenda kukagua Mradi wa maji wa Gararagua/Dachcona ambao unadaiwa kujengwa chini ya kiwango na kushindwa kutoa huduma.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Dancan Urassa, alieleza kuwa hivi sasa jitihada za makusudi zinahitajika kufanyika ili maji yapatikane na kuwaondolea kero wananchi, badala ya siasa kuvuruga mchakato unaolengwa.



Mkulima wa machungwa wilayani Muheza, mkoani Tanga, Solea Masanja (kulia), akionyesha kwa waandishi wa habari, baadhi ya matunda hayo, yaliyoharibiwa na inzi mharibifu shambani kwake jana, licha ya kutumia dawa mbalimbali kutoka kwa wataalamu wa kilimo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TCCIA yaanika yanayokwaza wanachama

**Na Dege Masoli,** KILINDI

CHAMA cha Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), kimeweka hadharani mambo tisa yanayotishia ustawi wa wanachama wake, ikiwamo kusuasua kupatikana kwa ufumbuzi juu ya mikataba ya kinyonyaji kwenye migodi ya madini.

Akizungumza jana katika kikao cha Baraza la Biashara la Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, Katibu wa TCCIA wilayani hapa, Kisyeri Daudi, alisema wameiandikia barua serikali ya kuwakumbusha kutafuta mwarobaini wa matatizo hayo ili kutowavunja moyo wafanyabiashara.

"Jambo la kwanza tunalotaka ufumbuzi wake ni kufumuliwa hii mikataba ya kinyonyaji katika machimbo ya madini hasa yaliyoko Kilindi.

"Maeneo ambayo wachimbaji wadogo wanaingia mikataba na wenye leseni kwa ajili ya uchimbaji, wanakumbana na ukiukwaji wa mkataba na mchimbaji mdogo anapofikia eneo lenye matumaini ya kupata madini, anapewa masharti magumu na hata kutishiwa kufukuzwa katika mashimo hayo," alisema.

Aidha, Kisyeri alisema wachimbaji wengi katika Wilaya hiyo, wanakadiriwa kodi ya juu na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakati uzalishaji haufanani na kodi.

"Pia kuna suala la miundombinu mibovu kwenye maeneo ya barabara za vijijini, uchakavu wa barabara ziendazo machimboni na miundombinu mibovu kwenye masoko na minada. Hayo yote tunatakata yapatiwe ufumbuzi wa kudumu," alisema.

Kuhusu matumizi ya vitambulisho vya ujasiamali, Katibu huyo alisema wanachama wao ambao ni wajasiriamali wanalipia pesa na upatikanaji wake unachukua muda mrefu na kwamba halina afya na linasababisha usumbufu mkubwa kwao.

Alisisitiza kuwa jambo hilo limekuwa kero sugu, kwa kuwa hali hiyo inatokea wakati mchimbaji ameshatumia gharama kubwa hadi kufikia hatua ya uzalishaji.

Mgogoro wa aina hiyo umeripotiwa kuwaathiri wafanyabiashara na wachimbaji wa madini wanaofanya kazi zao katika machimbo ya Seita Kijiji cha Mafulila, Kata ya Tunguli, Wilaya ya Kilindi.

Akijibu malalamiko hayo, Mwenyekiti wa Baraza hilo la Biashara, Abel Busalama, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, aliahidi kuyafanyia kazi malalamiko yote yaliyowasilishwa na TCCIA ili kuwezesha uzalishaji wa machimbo hayo uwe na tija kiuchumi.

# Ukosefu wa weledi chanzo biashara kufa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), limetaja sababu za biashara nyingi zinazofunguliwa na kufa ndani ya muda mfupi katika mkoa wa Kilimanjaro ikiwamo kukosekana kwa weledi juu ya uanzishaji na usimamizi.

Meneja wa SIDO Mkoa wa Kilimanjaro, Allen Mhidze, alisema ushahidi wa kitakwimu kuhusiana na anguko hilo, unaungwa mkono na utafiti uliofanyika dhidi ya wafanyabiashara na wajasiariamali wadogo.

Mhidze alikuwa akizungumza jana katika mji wa Moshi, wakati wa mkutano wa utambulishaji wa maendeleo ya biashara na watoa huduma (BDSP).

"Lengo letu la kuwakutanisha hapa ni kutambua na kutambuana na watoa huduma, wajasiriamali au wafanyabiashara na wenye viwanda vidogo ili kupunguza idadi ya kampuni na viwanda au biashara zinazokufa.

"Ndiyo maana SIDO ikaamua kuwakutanisha leo (jana) hapa ili kufanya utambulisho wa watoa huduma, waweze kuzisaidia kampuni zetu kufika mbali. Huduma za maendeleo ya biashara zitakwenda kuwasaidia utafiti, ushauri na maelezo sahihi ya namna ya kuiendesha hiyo biashara hadi kufikia kuuza bidhaa yake sokoni na kukabiliana na ushindani wa soko," alisema.

Kwa mujibu wa Mhidze, upokeaji wa maoni yanayotokana na mapokeo ya mkutano huo, yatalisaidia shirika kuandaa muongozo wa uanzishaji na usimamizi wa biashara, utakaowasaidia wafanyabiashara, wajasiriamali na wenye viwanda vidogo kuendelea kusalia sokoni.

Naye mjasiriamali Stella Mariwa, ambaye anazalisha unga wa lishe kwa kutumia mbegu za mchicha, alisema mwongozo utakaoandaliwa na kutolewa na SIDO, utawasaidia kwenda kwenye ushindani wa biashara, hasa kwenye masoko ya ndani ya nchi na nje ya nchi.

"Tunaomba Wizara ya Viwanda na Biashara, iwawezeshe watu wa maendeleo ya biashara ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa kusaidia wafanyabiashara, wajasiriamali na wenye kampuni kufikia malengo yao ya kibiashara. Tunaamini kwamba jambo hilo litasaidia kuongeza na kutanua wigo wa biashara nyingi zaidi kuanzishwa," alisema Stella.





## Waiangukia serikali kutatua mgogoro wao na mwekezaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa Mtaa wa Matuli Kata ya Mnadani jijini Dodoma wameiomba serikali kuingilia kati mgogoro wa ardhi uliopo kati yao na mwekezaji anayedai kumiliki zaidi ya ekari 350 katika eneo hilo, hali inayosababisha washindwe kufanya shughuli za maendeleo.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika eneo hilo kwa nyakati tofauti, wakazi hao walidai mwekezaji huyo amekuwa akichukua viwanja vya wananchi na kujimilikisha kwa vitisho.

Paul Bankiye, Diwani wa Ndachi, alisema wanashangaa kuona baadhi ya viwanja vimechukuliwa na kumilikishwa kwa mwekezaji huyo bila makubaliano yoyote na wakazi wa eneo hilo.

"Mimi kama kiongozi baada ya kuona kuna mkanganyiko wa viwanja, vingine vinasoma vipo ndani ya mradi na vingine havipo ndani ya mradi, ilibidi niende wizarani na ilionekana eneo halipo nje ya mradi, limepimwa, kuna bikoni na maeneo mengine kuna viwanja.

"Mkanganyiko ulikuja baada ya kuona kuna viwanja vingine vimemilikishwa taarifa tunazozifahamu viwanja vipo nje ya mradi ndipo nilipokwenda Jiji na kuambiwa aliyepima ni Malima na nilivyomtafuta alisema yeye hajapima ila ana viwanja zaidi ya ekari 350 na amenunua kwa wakazi mmoja mmoja wa eneo hili. Kinala Mwilafu, mkazi wa eneo hilo, alimtaka mwekezaji huyo kueleza maeneo hayo yote zaidi ya ekari 350 aliyouziwa na wananchi waliandikishana kwa kiongozi gani.

"Maana mimi ninavyofahamu ukiuza au kununua ardhi lazima kuwe na mashahidi, wanasheria na viongozi wa eneo husika sasa tumuulize yeye, alifuata huo utaratibu au ndo alikuwa anakuja kuwatishia watu na kununua maeneo kwa bei ndogo.

"Iko wazi wanaoleta migogoro hii ni watu wa Jiji kwani wao ndiyo wanaotengeneza hati na kuwapa watu viwanja sasa sisi watu wa eneo hilo la Matuli hatuhitaji watu wa Jiji waje kupima bila kuufuata uongozi, hatutaki ubabaishaji kama kuja kupima waje wataalamu kutoka wizarani," alisema

Akijibu malalamiko hayo, mwekezaji huyo, Leonard Malima alisema hajaiba maeneo hayo wala kumlazimisha mkazi yoyote ili kupata ardhi hiyo ya ukubwa ekari 350.

# Muswada Sheria Bima ya Afya kwa Wote wakwama kujadiliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUSWADA wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022 umeahirishwa kujadiliwa na kupitishwa kwenye Mkutano wa Tisa wa Bunge kutokana na kutokamilika kwa mashauriano kati ya serikali na Bunge.

Jana Muswada huo ulipaswa kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu ili wabunge wajadili na kupitisha.

Akitoa taarifa bungeni jijini hapa jana, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alibainisha kuwa katika orodha ya shughuli za jana, kulikuwa na hati za kuwasilishwa mezani na Waziri wa Afya na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii lakini hazikuwasilishwa kwa sababu Bunge na serikali wanaendelea na mashauriano juu ya mambo ambayo hawajaafikiana vizuri kwenye muswada huo.

Alisema Bunge halitautazama muswada huo ambao kwa mara ya kwanza ulisomwa katika mkutano uliopita na kupelekwa kwa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambao ulipaswa uingie bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kumaliza kazi ya kuitunga sheria, hadi pale kamati husika itakapofikia mwafaka na serikali.

"Mchakato huo umeahirishwa hadi hapo mashauriano yatakapokamilika, Kwa sasa wanaendelea na mashauriano katika hoja kadhaa ambazo zimeibuliwa na wabunge, wadau mbalimbali waliojitokeza katika kamati na nyingine. Serikali inaendelea kuzitazama namna bora ya kuwahudumia wananchi kwenye eneo hilo la Bima ya Afya kwa Wote," alisema.

Dk. Tulia alisema muswada huo utapelekwa bungeni mara watakapokuwa wameshakamilisha mashauriano hayo.

Muswada huo uliwasilishwa bungeni katika mkutano wa Bunge wa Nane uliofanyika Septemba mwaka huu baada ya kuahirishwa kwa miaka kadhaa.

Kuwasilishwa kwake kulikuja baada ya tamko la Rais Samia Suluhu Hassan alilolitoa Septemba 11 mwaka huu wakati akiwa katika Jubilee ya Miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA).

Tangu Oktoba 19 mwaka huu, Kamati ya Kudumu ya Bunge Huduma na Maendeleo ya Jamii ilianza kupokea maoni ya wadau kuhusu muswada huo ili kufanya marekebisho kadhaa kabla ya kupelekwa bungeni.

Hata hivyo, wadau mbalimbali wamekuwa wakikosoa baadhi ya vifungu vilivyopo katika muswada huo.

**YALIYOMO**

Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote unazitaka mamlaka nane zinazotoa usajili, vibali, hati au leseni kwa waombaji kuzingatia kigezo cha kuwapo uthibitisho wa uanachama katika skimu ya bima ya afya.

Mapendekezo hayo yamewekwa kufanyika kwa kuzingatia sheria zilizotungwa na Bunge pamoja na mamlaka zinazohusika na usimamizi au utoaji.

Muswada huo pia unazitaja mamlaka hizo kuwa ni zinazotoa leseni ya udereva, bima za vyombo vya moto, utambulisho wa mlipa kodi, usajili wa laini za simu, leseni ya biashara, hati ya kusafiria au viza, uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha tano, kidato cha sita na vyuoni na utoaji wa Kitambulisho cha Taifa.

"Kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni, mwajiri katika sekta ya umma na sekta rasmi binafsi atapaswa kumsajili mwajiriwa katika skimu ya bima ya afya ndani ya siku 30 tangu kuanza kwa mkataba wa ajira.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kulia), akikabidhi kitabu kinachoelezea mafanikio na mwenendo wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa Mkuu wa kitengo cha mahusiano ya Serikali cha Benki ya NMB, Vicky Bishubo, baada ya kukizindua Dodoma juzi. NMB ni miongoni mwa wadhamini wa kitabu hicho kilichoandikwa na watu mbalimbali nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfuko kusaidia waandishi mahiri wa vitabu wanukia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldof Mkenda amesema serikali kupitia wizara hiyo iko mbioni kuanzisha mfuko rasmi wa kusaidia waandishi mahiri wa vitabu nchini.

Amewataka waandishi hao waliopo nchini kuchangamkia fursa zinazotolewa ili kutoa maandiko makini yatakayoleta tija kwenye jamii.

Prof. Mkenda ambaye alimwakilisha Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Continuity with Vision the Roadmap to Success for President Samia Suluhu Hassan uliofanyika jijini Dodoma juzi.

Alisema kuwa katika uongozi wa Rais Samia, uandishi umeonekana na serikali sasa kuufanya kwa vitendo kwa kuanzisha tuzo ya Mwalimu Nyerere ili waandishi nguli ambao ni mahiri washiriki na kujipatia tuzo hizo. Alisema katika kitabu hicho ameona kimeandikwa na waandishi wengi na ndani yake kina vitu vingi ikiwamo masuala ya elimu.

Mwandishi wa kitabu hicho, Prof. Ted Maliyamkono, alisema kulikuwa na kila sababu ya kuandika kitabu hicho kwa kushirikisha watu mbalimbali ili kuwaeleza watanzania na dunia kwa ujumla mambo mengi na mazuri yanayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema katika kitabu hicho walizingatia mambo muhimu ya kisera na si kufanya tathmini ya utawala wake na kuwataka wananchi wasione udhaifu na upungufu wa kitabu kwa kuwa lengo kuu la chapisho hilo ni kuchangia uboreshaji wa sera za serikali.

Alisema kuwa ndani ya kitabu hicho, kumeonyesha Rais Samia amekuwa wa kwanza kutembelea nchi nyingi tofauti na wengine ili kufungua njia zilizofungwa milango ya biashara.

"Pia amekuwa kiongozi wa kwanza kufanya filamu ya Tanzania The Royal Tour na amekuwa mtendaji wa vitendo na si wa maneno na kwenye utawala wake amekuwa wa kwanza kuteua mawaziri wawili wanawake katika wizara mbili ambazo hazikuwahi kuongozwa na wanamke ambazo ni Ulinzi na ile ya Mambo ya Nje," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alisema kitabu cha Continuity with Vision the Roadmap to Success for President Samia Suluhu Hassan kinakwenda kujibu maswali ya watu wengi na makundi mbalimbali kuhusu hoja nyingi zilizomo kwenye jamii.

Awali Mkuu wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, Prof. Hozen Mayaya akizungumza kwenye uzinduzi huo, alisema Rais Samia ametekeleza kwa ufanisi miradi ya kimkakati kwa ajili ya wananchi wake.

Alisema kuwa mikakati hiyo ni pamoja na ushiriki wake katika filamu ya Tanzania The Royal Tour ambayo imeongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchini na kazi kubwa ya wananchi ni kuendelea kumwombea.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Umoja wa Vyuo vya Mashariki na Kusini mwa Afrikia (ESAURP), Ruta Mutakyawa alibainisha kitabu kimewashirikisha watu 45 kutoka vyuo vya elimu vya juu na kina kurasa 624 zeye sura 29.





## Mauzo ya mchanga, vibali yaingiza bil. 3/-

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar, imekusanya Sh. bilioni 2.97 katika kipindi cha miezi mitatu kutokana na mauzo ya mchanga na vibali.

Fedha hizo zimekusanywa kutokana na utaratibu wa usimamizi pamoja na kuimarika kwa mfumo wa kielektroniki wa maombi ya vibali vya Maliasili zisizorejesheka.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Shabaan Ali Othman, aliyasema hayo jana katika kikao cha utekelezaji wa programu za wizara kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu, katika kikao cha pamoja na Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi kilichofanyika kisiwani hapa.

Alisema usimamizi mzuri pamoja na kuimarika kwa mfumo wa kielektroniki wa maombi ya vibali vya maliasili zisizorejesheka umesaidia udhibiti wa mchanga na kwamba idara ya Nishati na Madini imeimarisha kikosi cha doria kwa dhamira ya kudhibiti uchimbaji holela wa mchanga.

Katika kuimarisha udhibiti huo, alisema kikosi cha doria pia kilipatiwa mafunzo ya ukaguzi wa vibali na leseni pamoja na kuwapatiwa vifaa vya mawasiliano ili kurahisisha mawasiliano kwa ajili ya kuleta ufanisi katika kudhibiti maliasili hizo.

Pia alisema idara ya nishati na madini ilitumia Sh. milioni 100 kuwalipa fidia wananchi 23 ambao mazao yao yaliathirika kutokana na shughuli ya uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka ikiwemo mchanga katika maeneo yao. Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Yahya Rashid Abdulla, aliiagiza wizara kukutana na Mkuu wa Wilaya na vijana wanaouza mchanga eneo la Taveta, ili kutafuta namna ya kudhibiti biashara hiyo katika eneo hilo.

Naye Mkurugenzi wa Nishati na Madini, Mhandisi Said Haji Mdungi, alisema watalifanyia kazi agizo hilo lililotolewa na kamati hiyo, kwa ajili ya kupata maoni mbalimbali ingawa idara ya nishati na madini inatumia sheria namba 3 ya mwaka 2015, Sheria ya Mazingira ya Zanzibar ambayo inamruhusu mtu kusafirisha maliasili zisizorejesheka na sio kuuza.

# Dk. Mwinyi aahidi kuongeza bajeti afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali itaendelea kuongeza bajeti katika sekta ya afya kadiri hali ya uchumi itakavyoimarika ili kuhakikisha inatoa huduma bora.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa ripoti ya ufuatiliaji wa mkataba wa Nairobi, kuhusu mkutano wa kimataifa wa idadi ya watu na maendeleo, wenye lengo la kusimamia utekelezaji wa makubaliano kuhusu utoaji huduma bora kwa kinamama na watoto, uliofanyika Hoteli ya Melia, Kiwengwa mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2022/23 serikali imeongeza bajeti kwa Wizara ya Afya kwa asilimia 8.3 kutoka bajeti iliyotengwa katika mwaka wa fedha wa 2019/20, ikiwa ni juhudi za kufikia azimio la Abuja la asilimia 15.

Ongezeko hilo la bajeti, alisema limeimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya katika nyanja tofauti, zikiwamo huduma za mama na mtoto, huduma za watoto na vijana pamoja na uzazi wa mpango.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, hivi sasa wananchi wote wanapata huduma bora za afya katika eneo lisilozidi kilomita tano kutoka makazi ya kudumu ya mwananchi, huku serikali ikiwa katika hatua za mwisho kukamilisha mpango wa bima ya afya.

Dk. Mwinyi alisema kwa msaada wa washirika wa maendeleo, serikali inaendelea kuandaa mfumo wa afya, kujenga miundombinu ya afya, kuajiri rasilimali watu na kupata bidhaa zaidi za afya ili kutoa huduma bora za afya mijini na vijijini.

Pia alisema alisema juhudi zinafanyika kuongeza upatikanaji wa elimu ya umri wa kujamiiana na uzazi kwa vijana wanaosoma na wasiosoma, ili kuzuia pamoja na kukabiliana na viwango vya juu vya vifo vya uzazi, magonjwa na mimba za utotoni ambazo zimekuwa zikiendeleea kujiri licha ya juhudi mbalimbali za serikali.

Alisema pia serikali anayoiongoza inafanyakazi kwa bidii kukomesha ukatili wa kijinsia wa aina zote, zikiwemo mimba za utotoni.

Alisema sheria, sera na mikakati iliopo imeimarishwa ili kuakisi malengo yaliowekwa katika ngazi za kimataifa, kikanda na kitaifa.

Naye Mwenyekiti Mwenza wa Kamisheni ya Ufuatiliaji Maazimio ya Mkutano wa Nairobi, Rais mstaafu Jakaya Kikwete, alisema wataendelea kufuatilia changamoto mbalimbali zinazozikabili nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuona jamii wakiwamo wanawake wanapata haki zote zinazostahili ikiwamo elimu kwa ajili ya kupambana na umaskini.

Mkurugeni Mkuu wa Shirika Idadi ya Watu la Umoja wa Mataifa, Natalia Kanem, alisema dunia inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo matokeo yake wanawake na watoto wanashindwa kupata mafanikio vikiwamo vikwazo vingi vinavyotokana na ukiukwaji wa haki za binadamu.

"Ripoti yetu bado inasisitiza suala la wanawake kupewa kipaumbele katika kuyafikia malengo yao ikiwamo ushirikishwaji wa ngazi za kisiasa, kupambana na ndoa za utotoni ambazo ni kikwazo katika kupata haki ya msingi ya elimu,' alisema.



Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimuapisha Abeda Rashid Abdallah kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Wizara yasifu ushiriki NGO katika kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Mifugo na Uvuvi imesema inathamini juhudi na mchango mkubwa unaofanywa na taasisi za kiraia kwa wananchi katika kuimarisha kilimo hasa kwa wakulima wa mboga.

Waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, alisema hayo jana katika hafla ya ugawaji wa vifaa kwa wakulima wa mradi wa viungo katika taasisi ya Community Forest Pemba ya Wete kisiwani Pemba.

Alisema taasisi hiyo inafanya juhudi kubwa kwa wakulima katika kuimarisha na kuboresha sekta ya kilimo ili kufikia malengo ya serikali pamoja na wakulima ikishirikiana na wafadhili mbalimbali katika kuleta maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Shamata alisema ni vyema wakulima hao wakavitunza na kuvienzi vifaa hivyo ili kutumika ipasavyo katika malengo yaliyokusudiwa sambamba na kuleta mafanikio na maendeleo bora kwa jamii.

Mradi wa viungo, alisema umekuwa mstari wa mbele katika kutatua changamoto kwa wakulima ambao wamejikita katika ukulima wa mboga na viungo hivyo wizara itahakikisha inafatilia kwa kina wakulima hao ili kufanikisha utendaji wao wa kazi unaenda sambamba na malengo ya serikali.

Alisema wizara itaendelea kushirikiana na wadau wa kilimo kaika kuhakikisha wanaongeza nguvu za uzalishaji wa mazao bora yanapatikana.

Mkurugenzi Mkuu wa Community Forest Pemba, Mbarouk Mussa, alisema mradi wa viungo, matunda na mboga una lengo la kusaidia azma ya serikali katika kuimarisha kilimo katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuongeza kipato cha wakulima wadogo.

Alisema mradi wa viungo umewasajili wakulima 25,907 Unguja na Pemba na wakulima 8,976 wamepatiwa mafunzo kupitia mashamba darasa ambayo huanzishwa na watalamu wa kilimo.

Mkurugenzi huyo alisema miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika mradi huo ni kuanzisha vitalu nane vya uzalishaji Miche ya matunda na viungo Unguja na Pemba ambapo kwa upande wa Pemba imezalishwa miche 28,156 ambayo ina thamani ya shiling 28156000 iliyogaiwa kwa wakulima bure kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

Naye Ofisa Mdhamini wa Kilimo, Umwagiliaji, Mifugo na Maliasili kisiwani Pemba, Dk. Suod Nahoda Hassan, alisema wakati umefika kwa wakulima kujikita zaidi katika uzalishaji uliobora.

Tuwafu Ali Issa, mkulima wa mboga kijiji cha Wingwi kisiwano humo, alisema mradi huo wa viungo, matunda na mboga umewaletea mabadiliko makubwa katika kilimo ambacho kimewapatia mafanikio makubwa na maendeleo bora ya uzalishaji mzuri katika kilimo chao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



**DIAMOND**
UKURASA 15





# ACHENI KUMKERA MOBETTO

UKURASA WA 16

YUKO WAPI ?

# SALUM ABDALLAH-5

## Mwanamuziki kutoka familia tajiri Mtunzi wa kibao 'Mkono wa Idd'





**Na Adam Fungamwango**

LEO tunamalizia historia ya mwanamuziki Salum Abdallah Yazidu (SAY) ambaye tangu mwanzo sehemu zote nne tumeelezea tangu kuzaliwa kwake, changamoto alizopitia, hadi kuwa mwanamuziki mkubwa Afrika Mashariki na Kati.

Sehemu hii tunaendelea na kipengele cha chanzo cha kifo chake cha kusikitisha kilichotokea mkoani Morogoro. Sasa endelea.

Usiku kucha ulikuwa wa maumivu makubwa, asubuhi mgonjwa alipelekwa hospitali akafanyiwa upasuaji ikagundulika alivunjika kiuno na mifupa kupasua kibofu cha mkojo, jambo ambalo kutokana na kuchelewa kugundulika lilikuwa ni baya sana. Kama saa 7 mchana alitolewa chumba cha upasuaji na wenzie waliokuwa wakisubiri wakaambiwa waende makwao wakale vizuri ili waje baadaye kutoa damu kwa ajili ya mgonjwa.

Wakatoka kwa furaha wakijua mambo yatakuwa mazuri. Walielekea kwenye klabu yao wakatengeneza chakula na kula kwa furaha. Kulianza hata kuwa na utani kuwa ,Mwarabu akipona atatoa kibao kikali cha tukio hili' ikumbukwe kuwa baba yake Salum alikuwa Mwarabu halisi ila mama yake mzazi ndiyo alikuwa mkazi wa Morogoro. Lakini ilipotimu saa kumi jioni taarifa ikaja kuwa Salum amefariki. Watu wakaanza kumiminika nyumbani kwake, wakakuta hata maiti imeshafikishwa kwake na imewekwa katika chumba kimoja ambacho kilikuwa kimetayarishwa kwa ajili ya fremu ya duka. Inasemekana baada ya Salum kufariki, daktari mkuu wa Mkoa aliendesha gari lake hadi nyumbani kwa Salum na kupaki nje na kuanza kulia jambo ambalo mara moja ndugu walielewa kuwa mambo yameharibika.

Ndugu waliweza kutayarisha sehemu ambayo watu waliojitokeza kuweza kuaga mwili wa Salum kwa mara ya mwisho.

Haikuchukua muda habari zilisambaa kwa kasi licha ya kwamba wakati huo hakukuwa na simu wala mitandao ya kijamii.

Ulinzi ukalazimika ukimarisha kwa kusaidiwa na polisi.

Kesho yake hali ilizidi kuwa ngumu wakati wa kusindikiza maiti kwenda makaburini ilikuwa kama kila mtu alikuwa akitaka japo abebe kidogo jeneza, hadi ikalazimu FFU wawepo kuleta amani.

Jeneza la Salum lilibebwa kutoka Nunge nyumbani kwa mama yake hadi Msamvu kwenye eneo alipozikwa, watu wakiwa wamejipanga mstari mrefu jeneza likipitishwa chini, mkono kwa mkono, hawakutumia gari.

Baada ya kifo chake kutokana na simanzi kubwa, Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) ilisimamisha kupiga nyimbo za mwanamuziki huyo kwa muda.

Zilianza kupigwa baada miaka miwili au mitatu kupita pale angalau mashabiki wa mwanamuziki huyo na bendi yake ya Cuban Marimba majozi na simanzi yalipoanza kupungua.

Miezi michache kabla ya kufariki mwamuziki huyo alitunga na kurekodi kibao cha 'Ewe Mola Wangu' ambacho kilionekana kama kilikuwa kinatabiri kicho chake. Tunamalizia makala hii na kibao chake hicho.

"Eee Mola wangu E Mola wangu, nivue na ya dunia, hao walimwengu, hao walimwengu, wanitafuta kwa madawa, wataka wadhulumu roho yangu, ili wapate furahiwa eee. Nami natoa salamu zangu, ningalimo mu dunia, kwa ndugu na jamaa zangu, za mapenzi na furaha, za kuwatoa uchungu ajali itakaponifikia ee.

Nahadithi ndugu zangu, nyuma waliobakia, waibeba maiti yangu huku wakinililia, ninashtakia Mungu nilotendwa mu dunia, na hao walimwengu nao watawafikia eee."

# UDAKU TU



# DIAMOND INAMA UFIKIRI..

HIVI karibuni mtandao wa YouTube uliondoa ngoma moja ya Mbosso katika uwanja wake wa kusikilizia muziki na kuibua hisia tofauti kutoka kwa wadau.

Mbosso ambaye ni msanii kutoka lebo ya Wasafi, alijikuta akipata kibano hicho baada ya wimbo wake 'Yataniua' kuenguliwa katika mtandao huo siku moja tu alipozindua EP yake mpya inayoitwa Khan.

Kwa ambao hawajafahamu sakata hilo, inadaiwa wimbo wa Yataniua, kuna vipande vimeingizwa ambavyo vinafanana na kila kitu na ngoma mbili za wasanii wawili tofauti.

Wimbo wa kwanza ni Adiwale wa msanii kutoka Afrika Kusini Young Stunna na ule wa msanii Asake wa Nigeria katika kibao chake cha Piace Be Unto You.

Katika vipande vyote vinavyodaiwa kuibwa ni vile alivyoimba Diamond Platnumz, hivyo kuongeza joto kutoka kwa mashabiki wa muziki.

Madai ya kuiba vipande vya nyimbo kutoka kwa wasanii wengine, imekuwa ikiwaandama wasanii kutoka Wasafi, jambo ambalo linaibua hofu hasa kutokana na lebo hiyo kuwa kinara wa kutengeneza nyimbo kali za Bongo Fleva.

Ukiachana na wimbo huo wa Mbosso, pia Zuchu amepata malalamiko kama hayo.

Kutokana na mfululizo wa malalamiko hayo, ni wazi uongozi wa lebo hiyo wanatakiwa kukaa chini na kuangalia ukweli wake ili kupata ufumbuzi wa kudumu.

Mchambuzi wa muziki, Abdul Shekunenge amesema kinacholalamikiwa na wengi lazima kuwe na chanzo chake, ni lazima Diamond na uongozi wa wasafi kutafakari na kupatia ufumbuzi wa kudumu.

"Wafanye utafiti nini chanzo cha malalamiko ya aina hii, kisha watafutie ufumbuzi ili kuhakikisha kile walichokichuma kwa miaka mingi hakishuki," amesema.

Ameongeza kwamba vipande hivyo vinavyolalamikiwa inawezekana ilikuwa ni ubunifu wake na kwamba kwa bahati mbaya imefanana tu, hivyo ni muhimu kutafakari na kufanya utafiti zaidi kabla ya kutoa ngoma kuepuka mifanano kama hiyo.

Ikumbukwe kuwa lebo ya Wasafi ni kubwa kwa Afrika Mashariki na bara lote kwa ujumla, hivyo kufanya kazi kwa umakini ni suala la kuzingatiwa ili kuendelea kuwa kinara katika tasnia ya muziki kwa muda mrefu.

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**@shamsaford**
Unaweza ukawa yeyote kwenye hii Dunia .Kuna bahati,kuna muda wa Mungu ,kuna huruma na upendo wa Mungu.USICHOKE kujitafuta ,usikate tamaa ukiwa hai kila kitu kinawezekana . Kila mtoto ana bahati yake usimfananishe mtoto wako na mtoto mwingine


**@amisamobetto**
Siku zote ukitaka kuwa mtu mwenye amani na akili iliyotulia basi nyamaza kana kwamba huelewi ..... na puuza kana kwamba huoni wala kusikia






**@heriethpaul**
Ustawi wa akili huanza na kuhisi yote. Mema, mabaya, yasiyoelezeka. Na kukua kutokana na uzoefu. Ninajiunga na @dkny kwa kuanzisha mazungumzo kuhusu afya ya akili na kutetea wale walioathiriwa na ugonjwa wa akili. Kwa hivyo unaendeleaje, kweli

**@ chuchuhansy**
Najua hata ikitokea nimeacha kuigiza basi nimewaachia muigizaji ambae 99% atacheza kama mimi inshallah





**@stevenyerere2**
Mzee lile Fataki au mshutiii aliopiga ki Aziz Stephan ni balaaaaa

BASI SAWA

## Vanillah Music alivyosugua benchi



BAADA ya kutambulishwa katika tasnia ya muziki, Vanillah Music, amesema ametumia mwaka mmoja kukubalika na kuaminiwa na Ali Kiba.

Amesema ndani ya kipindi hicho alifundishwa namna ya kuwa karibu na wenzake ndani ya lebo ya Kings Music, na kwamba amegundua sehemu aliyokuwepo ni sawa na chuo.

"Kaka Kiba amenifundisha mambo mengi kuhusu muziki, mwanzo nilikuwa mbinafsi kwa kila jambo lakini nashukuru hilo sasa limeondoka baada ya kuwa karibu naye," amesema Vanillah.

## Nuh Mziwanda usirudie tena



MKALI wa Bongo Fleva, Nuh Mziwanda, amesema watu wasimfikirie tofauti kutokana na kuvaa kwake nguo ya kike, kwani ilikuwa moja ya matayarisho yake ya kazi.

Nuh Mziwanda ameiambia PlanetBongo ya East Africa Radio kwamba kuvaa mavazi ya kike alikuwa na lengo la kuvuta watu kuwa tayari na EP yake mpya ya Wonders.

"Nilitaka kuwaweka tayari watu kupokea EP yangu, sijafanya kwa ubaya ilikuwa njia moja wapo ya kusukuma biashara yangu. Kitendo cha watu kunitukana ni tayari wanajua kuna EP yangu



## ACHENI KUMKERA MOBETTO

MWANAMITINDO na mwanamuziki wa kizazi kipya, Hamisa Mobeto; watu wanaomfuatilia kila kukicha wanajisumbua, kwa sababu maisha yake anayapanga mwenyewe. Mobeto amesema kutokana na tabia yake huwa hapati shida kuishi kama anavyotaka, licha ya kuzungukwa na watu wenye mitazamo tofauti.

"Nimechagua kuishi maisha yangu mimi na si vinginevyo ndiyo maana kila kukicha sichuji na sichukii hata kidogo, maisha yangu ni mazuri kwa maana nina furaha moyoni mwangu na nina amani siku zote," amesema Mobeto.

## FILAMU Mbagoni: Himaya ya Wachawi

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU hii inaitwa 'Mbagoni' inayoelezea himaya ya watu ambao kazi yao wakiamka mpaka kulala akili yao iko kwenye uchawi tu. Wanakaa kufikiria uchawi kiasi kwamba hakuna maendeleo yoyote yanayofanyika. Kwa bahati mbaya hata mfalme wao anachofikiria ni uchawi na kutoa makafara bila sababu za msingi.

Imechezwa na wasanii wengi ambao ni kila Narvotus Mayenga, Lairat Seif Ponza, Asha Mlela, Suzan Nguvumali, Ayoub Taffy, Halima Maulid, Rajab Jumanne, Dotto Matotola, Norvatus Mayenja, Ally Njenje, Elizabeth Yohana, Habiba Kipaga, Halima Maulid,wote hao wakiongozwa na mzee Fadhili Msisiri aliyeigiza kama mfalme.

Inaanza kuonyesha himaya ya Chilabumba kuna mtu mmoja aitwaye Tamba akiwa na mkewe Maiza. Wao wenyewe wanapendana, lakini ndoa yao haipendwi na watu wengine kwa sababu tu Maiza hazai. Wazazi, ndugu jamaa na marafiki wa Tamba wanamshauri aole mke mwingine, lakini Tamba mwenye anakataa.

Unatengenezwa mpango wa fumanizi feki na ndugu zake Tamba. Wanamtengeneza mwanaume ili akutane njiani na Maza wazungumze sehemu ambayo Tamba atapita ili akasirike na kumuacha. Hilo linafanyika na kwa kiasi fulani linafanikiwa kwani Tamba akakasirika na kumtimua mkewe nyumbani.

Akiwa njiani kuelekea kwao, Maiza anatokewa na mzimu ukimuambia kuwa kama tatizo ni kuzaa basi atapata mtoto.

Huko kwa mfalme nako kukawa na mpango wa



kumtoa mtu kafara, lakini sharti awe ni mwanamke ambaye yuko kwenye ndoa lakini hazai. Wakaamua kumsaka mke wa Tamba kwani yupo yeye pekee kwenye himaya hiyo. Akapelekwa kutolewa kafara, lakini halikukamilika kwa sababu aliokolewa na mzimu ule ule uliomwambia atapata mtoto.

Ndugu wa Tamba wanamshauri arudiane na mwanamke wake wa zamani Makaluwa ambaye alishawahi kuzaa naye mtoto akafariki. Tamba anakataa. Kwa sababu anakumbuka kuwa mtoto yule aliliwa nyama na bibi yake mzaa mama.

Kwenye himaya hiyo watu wengi ni walozi. Maiza anashika mimba, lakini mtoto anayemzaa aitwaye Mviko ndiye anayetumwa na mizimu kwenda kumaliza uchawi kwenye himaya hiyo.

Wachawi wanafanikiwa kumuua Maiza baada ya kujifungua, lakini mtoto ambaye naye alitaka kumuua, walishindwa na alipofika umri wa miaka 12 tu, akaanza kazi ya kuwasaka walozi wote kwenye himaya hiyo. Wote wakaisha, wakiongozwa na mama wa Makaluwa, mkuu wa wachawi, aliyekuwa akilazimisha Tamba amrudie binti yake.

Mviko aliirudisha himaya kuwa shwari, lakini akabaki wa baba yake Tamba, mama yake Maiza akiwa amefariki.





## Billnass ndoa kwake tamu

MWANAMUZIKI Billnass amewashauri wanandoa kuwa wavumilivu kutokana na wao kuwa chanzo cha kusambaratika kwa familia.

Billnass amesema tangu afunge ndoa na msanii mwenzake Nandy, amegundua wanandoa ndio husababisha kuyumba na hatimaye kuvunjika kutokana na kutoheshimiana na kufuata maadili.

Billnass na mkewe Nandy walifunga ndoa miezi mitatu iliyopita na ndoa inasemekana imeweka historia ya kutumia bajeti kubwa kuliko ndoa za mastaa wengine Bongo.

## 5 KALI ZA MAAFA, AJALI, VIFO

**Na Adam Fungamwango**

JUMAPILI iliyopita Tanzania ilipatwa na msiba mkubwa kutokana na ajali ya ndege kuanguka na kutumbukia kwenye Ziwa Victoria, ikisababisha vifo cha watu 19, huku kiasi cha abiria 24 wakiokolewa.

Ndege hiyo ya Kampuni ya Precision Air ilikuwa ikijaribu kutua kwenye Uwanja wa Bukoba bila mafanikio.

Kuna watu wamepoteza baba, mama, wake, waume, wapenzi na wachumba zao. Mmoja alikuwa anakwenda kutambulishwa ukweni. Mwingine ndiyo kwanza alikuwa ametoka masomoni. Familia nyingi zimepoteza watu waliokuwa wanawategemea. Ni msiba mzito wa taifa.

Kwa bahati mbaya sana wanamuziki na wasanii wa sasa hawatungi nyimbo za majanga kama haya.

Zamani wanamuziki walikuwa wanatunga nyimbo za aina hii na kubaki kumbukumbu isiyofutika vizazi kwa vizazi.

Leo tunaziangalia nyimbo zilizoimbwa na wanamuziki kwa ajili maafa, ajali kama ya ndege iliyotokea Bukoba mkoani Kagera na kusababisha vifo.

**Mbaraka Mwinshehe-Poleni Rufiji**

Wimbo huu ulirekodiwa kati ya mwaka 1974 na 1975 kutokana na mafuriko makubwa zaidi kuwahi kutokea kwenye historia ya Tanzania ya mto Rufiji.

Ilikuwa mwaka 1974 mafuriko hayo yaliyotikisa nchi, yalisababisha vifo vya watu wengi, mifugo na mazao kuteketea kwa maji.

Baada ya maafa hayo ambayo hadi leo yamebaki simulizi kwani pamoja na mafuriko mengine kutokea ya hapa na pale, lakini hayakuweza hata theluthi kulinganisha na yale ambayo yalisababisha watu kuondoshwa kwenye bonde la mto huo na kuanzishwa vijiji kama Ikwiriri, Muhoro, Mkongo, Kilimani, Mloka na Msona.

Mbaraka Mwinshehe aliingia studio za Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) na kurekodi wimbo wa kuwapa pole wakazi wa Rufiji na hata Ulanga, kwani nao pia mafuriko hayakuwaacha. Wimbo ukaitwa 'Poleni Rufiji.

"Poleni sana ndugu zetu wa Rufiji kwa maafa mliyoyapata, poleni ndugu wa Ulanga kwa hasara kubwa zilizotokea.

Mafuruko yamekuwa makubwa sana, majumba na mashamba yamefagiliwa, hakubaki kitu ila ni vifo na njaa zimewakuta," hayo ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo.

**Max Bushoke-Ajali ya Aminani**

Wakati kwenye ndege iliyoanguka Jumapili kulikuwa na mwanamke aliyekwenda kujitambulisha ukweni, katikati ya miaka ya 1980 kwenye Mtaa wa Mafere Kinondoni, Dar es Salaam, alifariki mwanamama mmoja kwa ajili ya gari.

Wanamuziki wa Orchestra Safari Sound (OSS) Ndekule ambao walikuwa na urafiki na mume wa mwanamke huyo wakaamua kumfariji jamaa kwa kumtungia wimbo waliouita 'Ajali ya Aminani'.

"Mola aiweke pema peponi roho yake, Aminani Mandari mpenzi sitomsahau. Atakumbukwa daima na ndugu na jirani zake, wa Mtaa na Mafere, mwanaye Mwanaidi, Mariam Amina na Haji hawachoki kumuwaza mama." Ni moja ya shairi kwenye wimbo huo utunzi wake Maximillian Bushoke.

**Msondo Ngoma Music-Ajali**

Kabla hajafariki dunia mwaka 2006, TX Moshi alitunga na kuimba wimbo 'Ajali'. Wimbo huu aliutunga na kuurekodi baada ya kupata ajali ta gari maeneo ya Mivinjeni, Keko Machungwa, Dar es Salaam. Ni ajali ambayo ilisababisha matatizo ya mguu ambayo ndiyo yalisababisha kifo chake.

Hata wakati akitunga na kurekodi nyimbo hizi, akiwa hata jukwaani alikuwa anakaa kwenye kiti.

**Zahir Ally Zorro-Makiwa**

Ni wimbo uliotungwa na Zahir Ally Zorro kuhusu mpenzi wake aliyefariki na kumuacha mkiwa. Anasema hatomsahau mpenzi wake Chiku kwa sababu amemtoka kimwili tu, lakini kiroho yupo na yeye.

**Marijani Rajab-Zuwena**

Marijani Rajab anaizungumzia ajali ya gari iliyotokea kwenye daraja la Salenda ambayo mpenzi wake Zuwena yumo.

Aliposikia alitoka mbio hadi hospitalini kwenda kumuona kama yu hai au amekufa. Kwa bahati alimkuta mzima. Sasa anafikiria sinjui ingekuwaje, au angefanya nini kama mpenzi wake angekufa ajalini.

BONGO FLEVA

# ‘Batarokota’ HURUMA YENU ITAMUOKOA



MWANAMUZIKI wa Injili Paskal Linda, maarufu kama ‘Batarokota’, sasa anatafuta huruma za Watanzania kuokoa maisha yake kuwa hatarini kutokana na tatizo la misuli kupasuka.

Botarokota ambaye anaimba muziki wa Injili kwa mtindo wa Hip hop, anapata matibabu katika hospitali ya Muhimbili ambako anahitajika kufanyiwa upasuaji wa misuli ya koo.

Akizungumza na BT, Botarokota amesema matatizo hayo yalianza mwaka 2020 akiwa mkoani Mwanza.

Katika fani ya muziki, alianza mwaka 1990 katika kundi la G ta Dunia la mkoani humo na kutoa albamu yao ya kwanza .One Day’ mwaka 1998, ikiwa na nyimbo 10.

Baada ya kujitenga na kundi hilo, mwaka 2014 alitoa singo yake inayoitwa ‘Wewe Shetani Mimi Uniache’.

Baada ya kutambulisha kibao hicho, ndipo matatizo yalipomuanza kwa kuonyesha dalili ya kutapika damu.

Katika kutafuta tiba ya ugonjwa huo alilazwa katika hospitali za mkoa wa Morogoro na Soukoture ya Mwanza, lakini hakupata nafuu.

Hatimaye mwanzoni mwa mwaka huu, alihamishiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, ambako huko baada ya kufanyiwa uchunguzi ilibainika mishipa yake ya chini ya koo ni dhaifu na kusababisha kupasuka.

Huko iligundulika kuwa mishipa chini ya koo inapasuka mara kwa mara kutokana na presha ya ini.

Amesema daktari amemwambia anahitajika kufanyiwa upasuaji wa koo na inahitajika kiasi cha shilingi 800,000.

“Mimi mwenyewe nimejiwekeza na kupata nusu ya gharama, kiasi kingine nawaomba Watanzania wanisaidie ili nifanyiwe upasuaji,” amesema Botarokota.

Ameeleza kwa watu watakaopenda kumsaidia watumie namba ya akaunti ya NBC, 011174022426 kwa jina la Paskal Beatus Linda au Exim Bank 0371001234.



## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**Town Classic Band**
Jana kwa mara ya kwanza baada ya kumaliza ‘listening part, walikuwa ndani ya ukumbi ya Kibozone Malamba Mawili Mbezi, leo Jumamosi watafanya vitu vyao katika ukumbi wa Buga Lounge Kimara.

**Twanga Pepeta**
Baada ya maonyesho jijini Mwanza wikiendi iliyopita, jana Ijumaa walikuwa ndani ya ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, kesho Jumapili watamalizia wikiendi katikati ya Gwambina Lounge, zamani TCC Club Chang’ombe.

**Orchestra Sikinde Original**

Bendi hii mpya iliogawanyika kutoka Sikinde, leo Jumamosi inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Beach, kesho Jumapili kama kawaida itakuwa katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**Tukuyu Sound Band**
Kila Jumapili humalizia wikiendi katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park, uliopo Ubungo kando ya Barabara ya Sam Nujoma.

**FM Academia ‘Wana Ngwasuma’**
Kama kawaida yao, siku ya Jumamosi hufanya vitu vyao katika ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, uliopo kando ya barabara ya Sam Nujoma.

**Kimokimo Band**
Wakiwa chini ya mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa huwa ndani ya ukumbi wa Mariot uliopo eneo la Extertanal jijini Dar es Salaam.

**Mambo Live Band**
Kila Ijumaa inafanya vitu vyake katika ukumbi wa The Crown Pub, kisha Jumamosi inakuwa ndani ya ukumbi wa Village Hotel.

**Waluguru Original**
Bendi hii yenye maskani yake mjini Morogoro, kila Jumamosi hufanya vitu vyake katika ukumbi wa Terminal Pub Msamvu na Jumapili itakuwa ndani ya ukumbi wa F2 Florida mjini humo.

**Mjengoni Classic Band**
Bendi hii ya jijini Arusha, leo Jumamosi itafanya makamuzi yake katika ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**Maina Band**
Bendi hii ikiwa chini ya Liston Maina, leo Jumamosi itafanya makamuzi ya nguvu na itakuwa ndani ya ukumbi wa Regancy Park, Mikocheni.



# AKOTHEE ANG'AKA KUDANGA

MWANAMUZIKI nyota wa Kenya, Akothee amekuwa na hasira baada ya kushutumiwa kwa tabia yake ya kubadilisha wanaume mara kwa mara.

Akothee ambaye ni mama wa watoto watano amevishtumu vyombo vya habari na wanamitandao kwa kumpa picha mbaya mbele ya jamii.

Mwimbaji huyo mwenye umri wa miaka 42 amesema tofauti na wanawake wengine, yeye amekuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume watano pekee ambao amewahi kuchumbiana nao.

"Nina miaka 40 na wanaume 5, hesabu jinsi nilivyo na nidhamu. Tena sitoki nje katika uhusiano wangu. Mimi huchumbiana na mwanaume mmoja mmoja, na mume wa mtu kwangu sawa na kidonge kichungu. Napenda mwanaume wangu tu," amesema kupitia ukurasa wake wa Facebook.

Akothee alitoa ufafanuzi huo wakati alipokuwa akijibu tuhuma za kuwahi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mzungu kutoka Afrika Kusini.

Amesema mwanamume huyo anayeonekana naye kwenye picha ambayo imekuwa ikisambaa kwenye mitandao ya kijamii, alikuwa ni mpambaji tu kwenye video yake ya muziki na hawakuwahi kuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi.

"Yupo kwenye ndoa yenye furaha na ana watoto. Kitu gani kibaya nyinyi? Mnaweza kuwa na akili? Mheshimu familia za watu," amesema kwa jazba.

Aidha, mjasiriamali huyo shupavu ameeleza kuwa yeye ni mfano wa kuigwa katika jamii, tofauti ni kwamba watu wengine hawajaangaziwa sana kama yeye kwa sababu wao sio watu mashuhuri.

"Mimi ni bora kuliko wanawake wanaotoka nje, sikubaliani na upuuzi. Sheria zangu ,kama sio za maana kwetu ,tunaacha. Sitakuwa na wanaume sita maishani mwangu nampenda mwanaume mmoja kwa wakati," amesema mwanamuziki huyo.

Kufikia sasa, Akothee amekuwa katika uhusiano na wanaume matano wanaojulikana. Aliwahi kuwa kwenye ndoa na Jared Okello ambaye ni baba wa binti zake watatu kabla ya kutalikiana na kuchumbiana na wazungu wengine wawili ambao alizaa nao mtoto wa kiume kila mmoja.

Baadaye alijitosa kwa aliyekuwa meneja wake, Nelly Oaks kabla ya kutengana katika hali ya kutatanisha mapema mwaka huu.

Kwa sasa amechumbiwa na mzungu kutoka Uswizi ambaye amembatiza jina Omondi.




## We Teni tattoo hadi kwenye meno?

MKALI wa muziki wa Nigeria, Teni amewataka mashabiki zake kuwa na furaha kwa sasa kutokana na kuwa na uwezo wa kuwabusu kwa meno yenye michoro.

Katika video fupi aliyosambaza mtandaoni Teni ameonyesha mchoro wake maarufu kama VVS ambao alidai kuwa una thamani ya mamilioni ya pesa.

Teni alijigamba mtu yeyote atakayepata bahati ya kumbusu ni lazima atajisikia furaha kutokana na mwonekano huo.



## Bad Boy usiige maisha

MSANII na kipenzi cha mashabiki wa Nigeria, Bad Boy Timz ameelezea maoni yake kuhusu kile anachoona kama shinikizo katika tasnia hiyo.

Maoni yake hayo ameyatoa baada ya mwimbaji maarufu wa BXNX, hivi karibuni kutumia naira milioni 40 kununua gari la kifahari la Mercedez Benz.

Kutokana na tukio hilo, Bad Boy Timz alirekodi video akiwaambia mashabiki wake kwamba lilikuwa linazidi kuwa na maisha ya kifahari.

## Wizkid kuwa kama Bob Marley

STAA wa muziki wa Nigeria Wizkid, amedokeza kuwa anasimamia kazi zake yeye mwenyewe ili kazi zake zidumu muda mrefu.

Amesema anataka kuwa kama nguli wa muziki wa reggae Bob Marley, ambaye ni mmoja watu anaowapenda na kuwa mfano kwake.

Wizkid alihudhuria tamasha la muziki kwa heshima ya Bob Marley, na kueleza limemtia moyo kuendelea kusukuma mbele juhudi zake.





## Burna Boy, Shakira watikisa

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Nigeria, Burna Boy, kwa mara nyingine amewaambia mashabiki wake namna anavyojivunia kufuatia kolabo yake na nyota wa kimataifa, Shakira.

Burna na Shakira pia wanashirikishwa kwenye kampeni ya Krismasi kwa kuonyesha mitindo ya mavazi ya kifahari.

Baada ya ujumbe wake huo kusambaa mitandaoni, idadi kubwa ya Wanigeria walivamia ukurasa wa msanii huyo na kumpongeza kwa furaha.

## Mwigizaji Nollywood nusura auawe

Meneja wa Hoteli moja nchini Nigeria, amemuokoa na kifo muigizaji wa Nollywood baada ya mpenzi wake kuweka sumu katika kinywaji chake.

Katika video zilizosambaa mitandaoni mwigizaji wa Nollywood nusura anyweshwe sumu na mpenzi wake, video hiyo ilionyesha wakati meneja wa hoteli alipotoka nje ya ofisi yake ili kumzuia mwigizaji wa Nollywood asinywe kinywaji chake kilichokuwa na sumu.

Video hiyo iliyosambazwa na mwimbaji Kelly Handsome, iliambatana na chapisho lake akiwaonya wanaume kuwa waangalifu na baadhi ya wanawake wanaolala nao na kujihusisha nao.Akifichuu kwake.



MAKALA

# Dunia inavyohangaika mabadiliko tabianchi

## •Afrika yashuhudia ukame, njaa, mafuriko

Na Mwandishi Wetu

NCHI za Afrika zimejikuta zikikumbwa na athari za moja kwa moja za mabadiliko ya tabianchi. Kuanzia kusini hadi kaskazini, mashariki mpaka Magharibi ya bara kote kumejitokeza athari hizo.

Moja ya athari mbaya na imekuwa ikitolewa mfano ni ukame mbaya unaoendelea kuzikumba nchi za Somalia, Ethopia na Kenya na kusababisha maafa makubwa kwa binadamu na wanyama.

Inaelezwa mamilioni ya watu wapo hatarini kupoteza maisha yao kwa kukosa chakula na maji, huku wanyama pori wameripotiwa kufa katika mbuga tofauti za nchini Kenya.

Rais wa Tanzania, Samia Shuluhu Hassan, ameungana na viongozi mbalimbali duniani katika mkutano wa kilele wa kujadili namna ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi nchini Misri ili kupata ufumbuzi wa kudumu.

Katika hutuba yake katika kongamano hilo, Rais Samia ameitaka dunia kuungana kukabiliana na changamoto hiyo, akisema majawabu yake ni lazima yawe ya kimataifa na kuwatolea wito nchi zilizoendelea ambazo ndio zinaongoza kwa uchafuzi zitekeleze kwa vitendo ahadi zao za kupunguza madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Amesema pamoja na nchi masikini ikiwamo Tanzania kujitahidi kuweka mikakati ya utunzaji wa mazingira, bado hatua hiyo haitoshi kama hazina fedha za kutosha kukabiliana na maengo waliyojiwekea.

Akitoa mfano amesema Tanzania na nchi nyingine za kipato cha chini zimeandaa mipango ya kina ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Wakati Rais Samia akionyesha njia hiyo, mataifa tisa makubwa nayo yametambulisha umoja wao wa kuzalisha nishati kwa njia ya upepo wa bahari.

Uingereza, Ujerumani, Marekani na Japan ni miongoni mwa nchi zilizotangaza kujiunga na muungano wa kushajihisha uendelezaji wa nishati ya upepo wa mawimbi ya bahari, kwa jina la GOWA.

Muungano huo ulioasisiwa kwa lengo la kuondosha vikwazo vya kupata nishati, ulianzishwa awali na Shirika la Kimataifa la Nishati Jadidifu (IRENA) Denmark na Baraza la Nishati ya Upepo Duniani.

Mataifa mengine yaliyojiunga na muungano huo katika mkutano huo ni Ubelgiji, Colombia, Ireland, Norway na Uholanzi.

IRENA na Shirika la Nishati Duniani (IEA) wanatabiri kwamba kufikia mwaka 2050, nishati itokanayo na upepo wa bahari itapindukia jigawati 2000 kutoka 60 za sasa, hatua ambayo itasaidia kuzuwia kupanda kwa joto kwa zaidi ya nyuzi 1.5 za kabla ya zama za viwanda.



Mjumbe wa mabadiliko ya tabianchi wa Ujerumani, Jennifer Lee Morgan, ambaye nchi yake ni ya tatu kwa kuzalisha HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/guterrestuchukue-hatua-za-pamoja-ama-tuangamie-sote/a-63672039" nishati hiyo duniani, anasema kuna mipango ya kuongeza utowaji wa nishati ya upepo wa mawimbi ya bahari kwa kiwango kikubwa.

"Bahari ya Kaskazini itageuka kuwa mtambo mkubwa kabisa na endelevu wa kuzalisha umeme na kuchukuwa nafasi ya gesi na mafuta kwa haraka." Anasema Waziri wa Nishati wa Ubelgiji, Tinne Van der Straeten.

**UINGEREZA KUTOA MIKOPO NAFUU**

Katika hatua nyingine, Uingereza imesema inapanga kutoa mikopo mipya kuzisaidia nchi ambazo zimeathirika zaidi kwa majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi.

Wizara ya fedha ya nchi hiyo imesema kwenye taarifa yake kwamba mikopo hiyo itajumuisha kipengele kinachowaruhusu wakopeshwaji kuacha kulipa madeni yao endapo nchi zitakuwa zimekumbwa na majanga hayo.

Shirika la ukopeshaji wa nje wa Uingereza (UKEF) ndicho chombo kilichokabidhiwa jukumu la mikopo hiyo, ambayo itatolewa kwa mataifa yenye kipato cha chini na visiwa vidogo vidogo.

Wizara ya fedha ya Uingereza inasema kwamba taarifa za kina juu ya mpango huo zitatolewa kwenye mkutano huu wa COP27.

"Nina fahari kusema kwamba Wakala wa Ukopeshaji wa Nje wa Uingereza ndiyo wa mwanzo kabisa duniani kutoa mikopo ambayo itasitisha malipo ya huduma ya madeni kwa nchi zinazokumbwa na majanga ya tabianchi na ya kimaumbile." Anasema Naibu Waziri wa Fedha wa Uingereza, James Cartlidge.

**WASIWASI WATANDA ULAYA**

Shirika la Mazingira barani Ulaya (EEA) linasema kuwa mabadiliko ya tabianchi yamegeuka kitisho kwa afya na mustakabali wa binadamu.

Linataja kiwango kikubwa cha joto, mafuriko, na moto unaowaka misituni inageuka kuwa uhalisia wa maisha ya sasa.

Mkutano huo wa Misri, shirika hilo linasema kulikuwa na idadi kubwa ya vifo kwenye majira ya kiangazi ya mwaka huu barani Ulaya vilivyotokana na kuongezeka kwa joto.

"Idadi hii inaweza kuongezeka endapo hakutakuwa na hatua za uhakika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi." linasema shirika hilo.



MAKALA

Na Mwandishi Wetu



# Maajabu damu sasa kuzalishwa maabara

## •Utafiti wabaini ni bora kuliko ya binadamu

TEKNOLOJIA inazidi kukua kwa kasi kiasi ambacho ni kawaida kuona nyama inaoteshwa kwenye maabara na viungo vilivyotengenezwa na binadamu kama njia ya kukidhi mahitaji ya kitabibu.

Hata hivyo, ulimwengu umezidi kushangazwa baada ya damu kuingia kwenye orodha ya viungo vinavyoweza kutengenezwa na binadamu.

Imeelezwa kwa mara ya kwanza dunia imeshuhudia damu iliyoundwa katika maabara imeweza kuwekwa kwa binadamu, hayo ni kulingana na watafiti kutoka nchini Uingereza.

Kama sehemu ya majaribio , kiasi kidogo cha vijiko viwili vya damu vilitiwa katika mwili wa binadamu.

Watafiti wanaona jinsi damu iliyotengenezwa kwenye maabara inavyofanya kazi baada ya kuingia mwilini.

Kundi la maafisa wa afya kutoka NHS Blood and Transplant ya Uingereza na wenzao wa Bristol, Cambridge walifanya kazi kwa pamoja kwenye mradi huo.

Kutokana na maumbile ya binadamu, kwa hakuna chaguo jingine bali ni lazima mtu anayeishiwa damu kutegemea watu wengine wamchangie.

**AINA ADIMU ZA DAMU**

Kupata damu kutoka kwa makundi adimu kama vile 'Bombay blood' na 'AB-ve' ni kazi ngumu sana. Lakini lengo kuu la watafiti ni kukuza makundi kama hayo kwa kuwapatia damu kutoka maabara.

Watu wanaougua magonjwa kama vile saratani ya damu maarufu kama selimundu mara nyingi huhitaji kutiwa damu ya kwenye mishipa.

Damu ya kundi moja la damu na mwili wa mgonjwa inapaswa kuongezwa. Ikiwa damu ni ya kundi tofauti, mwili hautakubali.

"Baadhi ya aina za damu ni nadra sana", anasema Prof Yasley Toye wa Chuo Kikuu cha Bristol.

Anasema kuwa ni watu 10 tu duniani wanaweza kuchangia baadhi ya vikundi.

'Bombay blood' ni mojawapo ya makundi ya damu adimu zaidi duniani. Ilitambuliwa kwa mara ya kwanza huko Bombay. Kwa sasa kuna vitengo vitatu pekee vya aina hii ya damu vinavyopatikana Uingereza.

Watafiti wanatumai kutengeneza damu katika maabara kama suluhisho la shida kama hizo.

**JINSI INAVYOANDALIWA**

Jinsi damu ya maabara inavyoandaliwa, ni pale seli nyekundu za damu zina jukumu muhimu katika kubeba oksijeni kutoka kwa mapafu hadi sehemu zingine za mwili.

Kwanza, karibu 470 ml ya damu hukusanywa kutoka kwa wafadhili, halafu seli za shina ambazo zina uwezo wa kuwa seli nyekundu za damu hukusanywa kutoka kwa damu kwa msaada wa shanga za sumaku.

Seli shina hizi hukuzwa kwa wingi katika maabara, kisha hubadilishwa kuwa seli nyekundu za damu.

Utaratibu huu wote unachukua kama wiki tatu. Hivi sasa, seli nyekundu za damu crore 5,000 zinazalishwa kutoka kwa seli za shina laki tano. Baada ya hapo, huchujwa katika hatua kadhaa na hatimaye chembe nyekundu za damu milioni 1,500 hukusanywa.

Chembe hizi nyekundu za damu crore 1,500 hukua na kuwa damu.

"Tunatumaini kutoa damu nyingi iwezekanavyo katika siku zijazo. Ndoto yangu ni kuwa na mashine kubwa inayoendelea kutoa damu,' aanasema Prof. Yasli Toi.

**DAMU BORA**

Mpaka sasa watu wawili pekee wamejitolea kuwekewa damu iliyotengenezwa na maabara.

Jumla ya watu 10 wenye afya njema watachangia damu kama sehemu ya utafiti huu. Kati ya mililita 5 hadi 10 za damu hutiwa katika miili yao kila baada ya miezi minne. Moja hupewa damu ya kawaida na mwingine ni damu iliyotengenezwa katika maabara.

Seli za damu zinazokuzwa katika maabara zimetambulishwa kwa nyenzo za mionzi. Kwa njia hiyo watafiti wanaweza kuona ni muda gani damu hiyo inakaa mwilini.

Damu iliyotengenezwa na maabara inadhaniwa kuwa na ufanisi zaidi kuliko damu ya kawaida.

Kwa kawaida chembe nyekundu za damu mwilini hufa ndani ya siku 120 hivi.

Baada ya hapo, wanapaswa kubadilishwa na kupata mpya. Wakati damu inakusanywa kutoka kwa mwanadamu, ina chembe nyekundu za damu changa na za zamani. Kwa hiyo baadhi ya seli nyekundu za damu hufa.

Lakini damu iliyotengenezwa na maabara ina chembechembe zote nyekundu za damu, kwa hivyo zinaishi kwa siku 120.

Watafiti wanasema, hakuna haja ya kuwekewa damu nyengine

Hata hivyo, kuendeleza damu katika maabara kunahitaji kushinda changamoto za kifedha na kiufundi.

Gharama ya wastani ya kuchangia damu kwenye NHS nchini Uingereza ni paundi 130. Lakini kuikuza katika maabara inagharimu zaidi.

Seli za shina zilizovunwa kutoka kwenye damu hufa haraka. Kwa hiyo, idadi ya kutosha ya seli nyekundu za damu haiwezi kutengenezwa. Kwa maana hiyo, kiasi kidogo cha damu kinatengenezwa.

Utafiti mwingi bado unahitajika ili kutengeneza damu ya kutosha kwa mahitaji ya binadamu.



MAKALA

# Kufufuka mauaji albino nani alaumiwe?

## •LHRC, TAS, watoa mbinu kukomesha

Na Sabato Kasika

NOVEMBA 2 mwaka huu, kuliripotiwa tukio la watu wasiojulikana ambao wanadaiwa kumuua mtu mwenye ulemavu wa ngozi (albino).

Mauaji hayo yanadaiwa kutokea katika Kijiji cha Ngula wilaya ya Kwimba, mkoa wa Mwanza.

Aliyeuawa na watu hao anatajwa kwa jina la Joseph Mathias (50), ambaye inaelezwa kuwa alikatwa mkono wa kulia na kuvuja damu nyingi hadi kumsababishia kifo chake.

Kufuatia tukio hilo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), kwa pamoja wametoa tamko la kulaani mauaji hayo.

Tamko hilo lililotolewa Jumatatu wiki hii, linakwenda sambamba na mapendekezo kwa serikali, polisi na wadau wengine.

Mapendekezo hayo, yanayolenga kulinda uhai wa watu wenye ulemavu, ni pamoja na jamii kuachana na mila potofu zinazochangia mauaji na badala yake itambue kuwa albino ni binadamu kama walivyo watu wengine.

"Kwanza tunaikumbusha jamii kuzingatia hilo kwamba watu wasiwe wepesi kuamini waganga wa kienyeji wanapowaagiza kuwadhuru binadamu wenzao, kwa ajili ya viungo hivyo," anasema Anna.

Aidha, anasema LHRC na TAS wanaunga mkono harakati zilizofanywa na Mkuu wa Mkoa Mwanza, Adam Malima ambaye ametoa siku saba polisi mkoani humo kuhakikisha wahusika wa mauaji hayo wanakamatwa.

"Wito wetu kwa serikali na polisi ni kwamba wahakikishe watuhumiwa wote wa kesi za mauaji ya albino wanakamatwa, upelelezi kufanyika kwa wakati na watuhumiwa kufikishwa mahakamani na kupatiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine," anasema.

Mbali na hilo, anasema ni vyema upelelezi upanuliwe ili wahamasishaji wa soko haramu la viungo vya albino wakiwamo waganga wa kienyeji wachukuliwe hatua kali za kisheri.

Anatoa ombi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana na Watu Wenye Ulemavu, kukamilisha mchakato wa upitishwaji wa rasimu ya mpango mkakati wa kitaifa kuhusu watu wenye Ualbino wa mwaka 2020/2024.

"Ikumbukwe kuwa rasimu hiyo ni zao la ushirikiano kati ya ofisi hiyo, taasisi mbalimbali za serikali na wadau wa asasi za kiraia uliodumu takriban miaka mitatu sasa tangu mwaka 2019," anasema.



Mkurugenzi wa Mtendaji wa LHRC Anna Henga (kushoto) na mwenzake wa TAS,Musa Kabimba. PICHA: SABATO KASIKA

Anafafanua kuwa endapo rasimu hiyo itapitishwa, serikali itakuwa na mpango mkakati thabiiti wa kukabiliana na madhila dhidi ya watu wenye ualbino na vikwazo vingine wanavyokumbana navyo.

"Tunaleta ombi lingine kwa serikali kuridhia Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu, uliopitishwa na Umoja wa Afrika mwaka 2018. Mkataba huu umetazama haki za watu wenye ulemavu katika mazingira halisia ya Kiafrika, ikiwamo kutambua changamoto za imani potofu zisababishazo madhila dhidi ya watu wenye ualbino," anasisitiza.

Mkurugenzi Mtendaji huyo pia anaigeukia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na asasi za kiraia kurudishwa upya juhudi za pamoja za kukemea ukatili na mauaji dhidi ya watu wenye ualbino na kutoa elimu kwa jamii kuhusu utu wa watu wenye ulemavu wa ngozi (albino).

Anasema miaka ya nyuma kulikuwa na ushirikiano kati ya tume hiyo na wadau wengine wa kutetea haki za binadamu, na kwamba tukio hilo liwarudishe pamoja ili kukomesha vitendo hivyo katika jamii.

**HALI YA MAUAJI**

Anna anakumbushia kuwa miaka mitano iliyopita, kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, hakukuwa na ripoti yoyote dhidi ya mauaji ya albino kutokana na juhudi za pamoja za jeshi la polisi na asasi za kiraia.

Anasema juhudi hizo pia zilihusisha mahakama na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Hata hivyo, kuanzia Mei mwaka jana, kulitokea mauaji ya mtoto huko mkoani Tabora.

"Mwili wa mtoto huyo uliokotwa ukiwa umekatwakatwa viungo mbalimbali vya mwili wake ukiwamo mkono. Lakini pia Novemba mwaka huo huo, kulitolea mauaji mengine ya mtu mwenye ualbino," anaeleza.

Anna anasema mauaji hayo yalitokea wilayani Lushoto mkoani Tanga, kufuatia mwili wa mtu aliyemtaja kwa jina la Heri Shekighenda aliyekuwa amezikwa, ulifukuliwa na kunyofolewa viungo vyake.

Aprili mwaka huu, kituo kimoja cha televisheni kiliripoti tukio la Mohamed Rajabu mkazi wa Mabibo Dar es Salaam alivamiwa na watu wasiojulikana na kukatwa panga lakini hawakufanikiwa kutimiza lengo lao.

Mbali na matukio hayo, anaongeza kuwa Julai mwaka huu, kulitokea tukio lingine Wilaya ya Shinyanga Mjini, ambapo Eunice Zablon alifuatwa na mtu mmoja aliyemuomba kinyesi cha albino, kwa ajili ya kukiuza.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), Musa Kabimba, anawataka wenye ulemavu huo kuendelea kuchukua kila aina ya tahadhari kwa ajili ya usalama wao.

Anataja tahadhari hizo kuwa ni pamoja na kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola wanapoona viasharia vya ukatili huo au kuona mtu ambaye hawamuelewi vizuri akizunguka kwenye maeneo yao.

Kabimba anasema njia hiyo inaweza kusaidia kukomesha vitendo hivyo vya kikatili vinavyochangia kuondoa uhai wa watu wasio na hatia, kwa sababu ya tamaa ya kutaka utajiri kwa njia ya mkato.

"Nani anawadanganya kuwa viungo vya albino vina uhusiano na utajiri, kuna haja kwa serikali kuwa na mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ya kukabiliana na watu wanaoua albino," anasema Kabimba.

Kabimba anaongeza kuwa katika mazingira hayo ya mauaji ya albino yanaweza kusababisha uwekezaji kuwa mgumu, kwa madai kwamba wawekezaji hawawezi kwenda kuwekeza kwenye mazingira ambayo kuna ukatili wa aina hiyo.



Baadhi ya watoto wenye ulemavu wa ngozi.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Vituko vya abiria wa mabasi ya Ikarus

## ■Ni mwendokasi ya miaka ya ‘70 yaliyosababisha kiwewe kwa Wabongo

**Na Adam Fungamwango**




MWISHONI mwa miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1980, Tanzania ilipokea mabasi kutoka nchini Hungary. Kama itakumbukwa ni kwamba ilikuwa ni moja kati ya nchi za mfumo wa kijamaa, hivyo haikuwa ajabu kwa nchi hiyo kuipatia Tanzania mabasi kwa sababu zote zilikuwa zinafuata mrengo huo.

Aina hii ya mabasi ilikuwa ni tofauti na yale ambayo tuliyoyazoea kuyaona. Kwa kizazi hiki sitaki kuzunguka sana, bali ni kuwaambia tu yanafanana na mabasi ya mwendokasi yale marefu yenye tela, au kama ambavyo picha inavyoonyesha.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa wananchi wa Tanzania kuona mabasi ya aina hiyo, hivyo ni mabasi yaliyokuwa si tu kivutio, lakini yalisababisha vituko vingi.

Mara ya kwanza ilikuwa ni mwishoni mwa miaka ya 1970 yalipoingia, lakini pia baadaye yalikuwa yakiingia kwa awamu tofauti, lakini hadi kufika katikati ya miaka ya 1980, mabasi hayo yalikuwa mengi jijini Dar es Salaam.

Mabasi hayo yaliitwa Ikarus na siyo kwamba yalikuwa mali ya mtu binafsi la hasha, yalikuwa ni mali ya serikali chini ya Shirikika la Usafiri Dar es Salaam (UDA).

Kwa maana hiyo mabasi hayo yalikuwa yanafanya safari zake Dar es Salaam tu, wala hayakuwahi kwenda kwenye mikoa mingine. Wakazi wa mikoa mingine waliyaona wakija Dar tu.

Sifa yake ya kwanza ni kwamba ilikuwa inachukua abiria wengi kwa wakati mmoja. Hata kama kuna abiria wengi kituoni, basi likija, kama siyo wote, lakini idadi kubwa ya abiria itakuwa imechukuliwa.

Ndiyo maana watoto wa mjini wakayabatiza jina na kuyaita ‘kumbakumba’, yaani ni kwamba likifika hata moja tu linakumba watu wote kituoni.

Mabasi hayo yalisaidia sana maeneo ambayo yana shida ya usafiri, ingawa kulikuwa na matatizo kadhaa ambayo nitayaeleza baadaye.

Sifa nyingine ni kwamba ndiyo yalikuwa mabasi mazuri sana ukiwa ndani, unaweza ukadhani kama uko kwenye ndege, tofauti na aina nyingine ya mabasi.

Dereva alikuwa na kipaza sauti ambacho anaweza kuwasiliana na abiria waliomo ndani na kondakta wake. Aliweza kuwaambia wafunge vioo, au kusogea ambapo anaona panafaa kufanya hivyo.

Viti vyake, mandhari yote ya ndani ambavyo abiria wengi walikuwa hawajawahi kukutana navyo, walijiona kama wako peponi wanapokuwa ndani ya mabasi hayo.

Sifa ya tatu mabasi hayo yalikuwa mapana tofauti na aina nyingine ya mabasi, madirisha makubwa, hivyo yaliweza kuingiza abiria wengi na hewa. Ikumbukwe pia yalikuwa na vipoza hewa pia maarufu kama AC.

Springi zake au shokamzoba zilikuwa laini tofauti na aina nyingine ya mabasi kiasi kwamba linapopita sehemu ambayo ina mashimo kidogo, tuta au kibonde, inanesanesa kwa namna ya kumpendeza mtu yeyote anayekuwa ndani na si kukita chini na kuwa kero kwa abiria.

Kutokana na sifa hizo na zingine ambazo hazikuandikwa hapa kulikuwa na vituko vingi vya abiria kuhusu Ikarus.

Kwanza kuna watu, hasa vijana au watoto wakati huo anaweza kutafuta pesa kwa ajili ya kutaka kupanda tu Ikarus, aende nalo mjini Posta, Stesheni au Kariakoo halafu ageuze nalo. Mtu hana safari yoyote lakini anachotaka yeye ni kupanda tu basi hilo.

Wengine ambao wana safari lakini hawana haraka walikuwa hawataki kupanda basi lolote lile zaidi ya Ikarus. Atakaa hata masaa mawili kituoni, lakini analisubiri hilo tu.

Kutokana na ugeni au ‘ushamba’, baadhi ya abiria walikuwa wanaogopa kukaa kwenye tela lake la nyuma, wakidhani kuwa linaweza kukatika katikati, la mbele likaendelea na safari na la nyuma likabaki na kuwaletea matatizo.

Wapo wale watoto wa mjini, wao walipopanda mabasi hayo walipenda kwenda kukaa katikati ya maungio.

Katikati ya maungio chini kulikuwa na sahani kubwa ambaye inaonekana kuzunguka likikata kona, lakini pembeni yake kwenye mipira ya maungio kuna machuma fulani yaliyotengenezwa kama kuzuia watu kugusa mipira ile.

Watoto wa mjini walikuwa wakikaa juu ya machuma yale na mambo yakawa yanaendelea kama kawaida.

Hata hivyo, kuna mapungufu ambayo nilisema nitayaeleza. Mabasi hayo yalikuwa yakifanya safari zake kwenye barabara ambazo ni nzuri na zenye ubora kwa jinsi zilivyotengenezwa, hivyo hazikupelekwa kwenye maeneo ambayo hakukuwa na barabara bora. Kumbuka kuwa zamani barabara bora za lami zilikuwa chache sana tofauti na sasa.

Pia hazikupelekwa sehemu ambazo zina kona kali sana kutokana na jinsi zilivyo ndefu, na hakutakiwa kukata kona nyingi za mara kwa mara hasa zile kali. Kwa maana hiyo Ikarus zilikuwa zinafanya kazi maeneo machache tu, lakini sehemu zingine zilikuwa hazifiki, hivyo kuwa lulu na kuhitajika sana na abiria waliokuwa wakizitafuta ili tu wapande na wao wawe na cha kusimulia.

Bendi iliyomilikiwa na shirika hilo iliyokuwa ikiitwa UDA Jazz, ilitumia mtindo wa ‘Ikarus Kumbakumba’ kama vile ilivyo Sikinde Ngoma ya Ukae au Msondo ngoma kutokana na mabasi hayo.

Hebu sasa tuangalie baadhi ya meseji za wadau baada ya mada hii kuwekwa kwenye mtandao ili achangie.

“Kipindi cha mabasi hayo yaliweza kumudu huduma ya Dar, tatizo ilikuwa huduma, hasa spea mafundi waliopelekwa Hungary kusomea waliporudi wao wakawa watu wa ofisi tu hawashiki spana,” alisema mmoja wa wachangiaji.

“Aisee hayo mabasi yalikuwa imara sana kitu cha Hungary enzi hizo, ukiendesha hilo gari basi unaishi Masaki kota za UDA, unapewa heshima zote ukija kwetu Magomeni uswahilini.” Akaongeza mchangiaji mwingine.

“Nakumbuka tiketi za msimu, ukiwa nayo wewe ni kulivinjari tu jiji la Dar, unaenda mahali popote kwa hiyo tiketi yako hadi muda wake uishe, umenirudisha mbali sana.” Mdau mwingine akaandika.



**Tuma meseji 0716 35053**

HABARI KIMATAIFA

# Joe Biden kuwasili Misri kuhudhuria COP27

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden, amewasili jana kwenye mji wa mwambao wa Sharm el-Sheikh nchini Misri kuhudhruia mkutano wa kilele wa Mabadiliko ya Tabianchi wa COP27.

Mkutano huo unalenga kutafuta makubaliano ya kudhibiti athari za kuongezeka kwa kiwango cha joto duniani. Wajumbe wa mkutano huo wanataraji uwepo wa rais Biden utaongeza nguvu katika kusukuma malengo ya dunia kwenye kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi licha ya matatizo yanayoukabili ulimwengu ikiwemo vita na uchumi unaochechemea.

Biden anatarajiwa kutumia hotuba yake mjini Sharm el-Sheikh kuyakumbusha mataifa duniani umuhimu wa kuendelea na mipango ya kupunguza utoaji wa gesi ya ukaa na kudhibiti kupanda kiwango cha joto kupindukia nyuzi 1.5 katika kipimo cha Celsius.

Wakati wa ziara hiyo ambayo ni kituo chake cha kwanza cha ziara ya wiki moja ya kimataifa, rais Biden anatazamiwa kutangaza mipango ya pamoja na Umoja wa Ulaya kudhibiti utoaji wa gesi chafu. **DW**

# Marais China, Marekani kukutana

**BEIJING,** CHINA

CHINA imethibitisha jana kuwa kiongozi wa nchi hiyo Xi Jinping atakutana na mwenzake wa Marekani Joe Biden, wiki inayokuja.

Mkutano huo utafanyika pembezoni mwa mkutano wa kilele wa kundi la mataifa tajiri na yale yanayoinukia kiuchumi la G20 utakaofanyika nchini Indonesia.

Taarifa hiyo ilitolewa na msemaji wa wizara ya mambo ya kigeni wa China ambaye pia amearifu kwamba rais Xi atakuwa na mazungumzo na viongozi wengine ikiwemo wa Ufaransa, Senegal na Argentina.

Ikulu ya Marekani tayari ilithibitisha hapo jana kuwa Rais Biden atakutana na Xi Jumatatu inayokuja kwa mazungumzo yao ya kwanza ya ana kwa ana tangu Biden alipochaguliwa kuwa rais wa Marekani.

Washington ilisema mazungumzo hayo yatagusia njia za kuimarisha ushirikiano kati ya China na Marekani pamoja na kuyatafutia majibu masuala yanayotatiza uhusiano baina ya madola hayo mawili ikiwemo hadhi ya kisiwa cha Taiwan. **DW**



Mtoto akimuongoza punda aliyebeba mizigo katika jimbo la Tigray hivi karibuni. Eneo hilo linakabiliwa na ukosefu wa chakula kutokana na vita. **PICHA: DW**

# Russia yajiondoa rasmi Kherson, yasisitiza itabaki kuwa mali yake

**MOSCOW,** RUSSIA

RUSSIA imesema kwamba bado inachukulia Kherson kuwa sehemu yake, licha ya kuamuru vikosi vyake kuondoka katika mji huo.

Katika taarifa iliyotolewa na msemaji wa serikali ya nchi hiyo, Dmitry Peskov, alisema hawaoni kama jambo la kufedhehesha kutokana na kitendo cha kuondoa vikosi vyake.

Peskov alisema kuondolewa kwa wanajeshi wa Russia kutoka Kherson hadi ukingo wa mto Dnieper haitabadilisha hali ya eneo la Kherson lililoshikiliwa na nchi yake.

"Hili ni somo la Shirikisho la Russia, hali hii inafafanuliwa kisheria na kulindwa. Hakuna na hapawezi kuwa na mabadiliko yoyote hapa," aliwaambia waandishi wa habari.

Peskov alikataa kujibu swali kutoka kwa waandishi wa habari kuhusu jinsi Vladimir Putin alichukua ripoti ya Jenerali Sergei Surovikin kuhusu hali ya Kherson na uamuzi wa Waziri wa Ulinzi Sergei Shoigu kuondoa kikundi cha kijeshi kutoka jiji hilo.

"Kulikuwa na uamuzi wa Waziri wa Ulinzi, kwa hivyo nakuomba uwasiliane na Wizara, sina la kusema juu ya mada hii," alisema Peskov.

Akijibu swali kutoka kwa BBC, Peskov alisema kuwa Russia haioni fedheha kuondoka kutoka Kherson.

Wakati huo huo, taarifa zinaeleza Russia imeondoa vikosi vyote kutoka mji wa Kherson.

Asubuhi ya jana, picha zimeonekana kwenye mitandao ya kijamii zikionyesha sehemu kadhaa zilizoharibiwa kwenye daraja pekee la barabara nje ya Kherson.

Hilo liliwafanya wanablogu wanaofuatilia kwa karibu vita hivyo kusema kujiondoa kwa Russia kutoka ukingo wa magharibi wa mto Dnipro kumekwisha.

Wizara ya ulinzi ya Russia iliyotajwa na shirika la habari la Tass, imethibitisha kwamba wanajeshi wote kwenye ukingo wa magharibi wamevuka upande mwingine.

Uamuzi wa kurudi nyuma ni pigo kubwa kwa jeshi la Russia katika kukabiliana na shambulio la Ukraine.

Rais Vladimir Putin, hakushiriki katika tangazo hilo la televisheni. Wizara hiyo ilisema Ijumaa kwamba hakukuwa na hasara ya wafanyakazi, silaha au vifaa vya kijeshi na kwamba hakuna vifaa vilivyoachwa nyuma.

Jeshi la Ukraine linasema limepata mafanikio makubwa katika siku ya mwisho karibu na Kherson, baada ya Russia kusema kuwa inajiondoa katika mji huo wa kusini.

Wanajeshi wa Ukraine walisema wameukomboa mji muhimu wa Snihurivka, kilomita 50 kaskazini mwa Kherson.

Serikali ya Ukraine pia imedai kuweka shinikizo kubwa kwa pande mbili karibu na Kherson, pamoja na kupiga hatua kilomita saba katika baadhi ya maeneo.

Russia inasema imeanza kuondoka katika jiji hilo - lakini mchakato huo unaweza kuchukua wiki.

Tangazo la Jumatano lilitazamwa kama kikwazo kikubwa katika juhudi za vita hivyo, ijapokuwa maofisa wa Ukraine walikuwa na mashaka wakionya kwamba ujanja huo unaweza kuwa mtego.

Katika hatua nyingine, Marekani na Uhispania zimetangaza zitatuma mifumo na makombora yake.

Mshauri wa kitaifa wa masuala ya usalama nchini Marekani Jake Sullivan, alitangaza kwamba Marekani itaipatia Ukraine mifumo ya Avenger ambazo ni silaha za kukabiliana na mashambulizi ya anga.

Avenger ni bunduki zinazofyatua makombora ya aina ya Stinger, ikiwa ni mifumo ya ulinzi ya masafa mafupi.

Idadi ya mifumo hii mipya itakayopelekwa Ukraine bado haijaelezwa.

Kulingana na Sullivan, Marekani pia itatuma makombora kwa Ukraine kwa ajili ya mifumo ya ulinzi ya Hawk.

Uhispania iliahidi kutoa msaada wa aina hiyo mpya wa mifumo ya ulinzi zaidi ya mifumo mingine miwili ambayo tayari iliikabidhi Ukraine.

Kulingana na Shirika la habari la Ukriform lililonukuu vyombo vya habari vya Ukraine msaada wa Uhispania ulitangazwa na Waziri wa Ulinzi, Margarita Robles katika mkutano na wanajeshi wa Ukraine ambao wanapewa mafunzo nchini Uhispania. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**TUSAJIGWE MAROBHE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0938-0583** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **MBEZI BEACH HIGH SCHOOL** mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHU/RB/372388/2022.**

---

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI GEITA**
**GEITA**
**MAOMBI YA JINAI NO. 04 YA 2022**
**JAMHURI....................................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**
1. **MARIAM D/O MWAKAPILA**
2. **PHILIPO S/O DAHAYE**
3. **FRANSIS S/O GOSBERT@ KAZAULA**
4. **FURAHA D/O HARISON............................WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA:**
1. **MARIAM D/O MWAKAPILA wa Mwatulole Geita**
2. **PHILIPO S/O DAHAYE wa Kalangalala Geita**
3. **FRANSIS S/O GOSBERT@ KAZAULA wa Kalangalala Geita**
4. **FURAHA D/O HARISON wa Ilemela Mwanza**

**UNAAMRIWA** na Mahakama hii kwamba ufike Mahakama ya Hakimu Mkazi GEITA mnamo tarehe 28 Novemba 2022 siku ya Jumatatu saa tatu kamili asubuhi ambapo shauri limepangwa kutajwa.
**ELEWA KWAMBA** ukikosea kufika siku hiyo shauri hilo litapangwa kusikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
**HATI HII IMETOLEWA,** kwa amri yangu iliyotolewa mnamo tarehe 14 Septemba, 2022.
**IMESAINIWA** hapa GEITA leo tarehe 10 mwezi Novemba, 2022.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
GEITA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA- MWANZA**
**SHAURI NA 253 LA 2022**
**LWEMPIS GENERAL CO. LIMITED...............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**AGNESS ALPHEUS SURUSI.........................MJIBU MAOMBI**

**KWA: AGNESS ALPHEUS SURUSI**

Unafahanmishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 15/11/2022 katika Chumba cha baraza, Barabara ya Makongoro jengo liko mkabala na Mahakama ya Mwanzo Mwanza mjini na Mahakama ya Wilaya ya Nyamagana, Tanzania.
Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- Ukijua kwamba ukishindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyie kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 11/11/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA- MWANZA**
**SHAURI NA 252 LA 2022**
**LWEMPIS GENERAL CO. LIMITED.........MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**MOHAMED IBRAHIM.........................MJIBU MAOMBI**

**KWA: MOHAMED IBRAHIM**

Unafahanmishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 15/11/2022 katika Chumba cha baraza, Barabara ya Makongoro jengo liko mkabala na Mahakama ya Mwanzo Mwanza mjini na Mahakama ya Wilaya Nyamagana, Tanzania.
Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- Ukijua kwamba ukishindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyie kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 11/11/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 2186/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HUSSEIN MSHAM HEMEDY**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SHAMIM HEMED**

### TANGAZO

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi wa 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 10 Mwezi wa 11 Mwaka 2022.

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**VICTOR ERASTO LAMECK** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3046-0162** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **MIRONGO SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **KAK/RB/1457/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA DODOMA**
**SHAURI LA MIRATHI NA.8/2022**
**CHRISTINA HONEST MASSAWE**
**WALTER HONEST MASSAWE ................... WAOMBAJI**
**HONEST DISMIS MASSAWE .................. MAREHEMU**

**KWA: YEYOTE,**
**POPOTE PALE ULIPO.**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI NA 8/2022 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA MAREHEMU HONEST DISMIS MASSAWE**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama kuu Tanzania, Kanda ya Dodoma, mbele ya Mhe. Jaji A. S. KAGOMBA, wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma,saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya jumatatu tarehe 15/11/2022
**HIVYO BASI;** unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO;** hutofika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo
**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 mwezi wa Oktoba,2022.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MULEBA MKOA KAGERA**
**MAOMBI MADOGO NA. 76/2022**
**PHARIDA SAID .....................................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**MASANSA LUSATO ................................MJIBU MAOMBI**

**KWA: MASANSA LUSATO (POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa maombi Na. 76/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 25/11/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, J.K. Banturaki saa 2:30 asubuhi, mahali - Muleba (Mamlaka ya Mji Mdogo).

Hivyo, unaamriwa kuhudhuria mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 07/10/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MULEBA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIZABETH GODFREY MLAGAZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 137 AAM.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/439055/2022.**

---

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, ni mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-5

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Sura yake ilikuwa ya mviringo, mashavu yake yalikuwa na vishimo ambavyo hujulikana sana kama 'dimpozi' hasa anapocheka.

Mdomo, macho yake ya duara, pua ni baadhi ya vitu vingine vilivyowafanya wanaume wengi kuchanganyikiwa.

Alikuwa ni mwembamba, lakini hipsi zake zilitengeneza daraja katikati kiasi cha kuonekana kama mcheza sinema maarufu duniani.

Anapotembea mwendo wake anakuwa kama mwanamitindo hivi. Ngozi wake maji ya kunde na ya kuvutia na kung'aa, lakini pia anapocheka meno yake yalionekana kujipanga vema kama punje za mahindi zilizojaa kwenye bunzi lake.

Kifupi tu uzuri wa binti huyo ulionekana kumpendeza Adel Adam, ambaye alitoka jijini Dar es Salaam akiwa hajabahatika kupenda mwanamke yeyote, lakini ghafla alionekana kumkubali Mary.

Alitamani masaa yasonge mbele haraka ili asubuhi ifike akamtafute msichana huyo. Alijiona mwenye bahati sana kukutana naye mchana. Lakini alijikuta asiye na bahati baada ya ahadi yake aliyo shindwa kutekeleza.

********************************

Alikuwa ameshaanza kukizoea kijiji hicho. Ilikuwa ni saa 11:00 jioni ukali wa jua ukianza kupungua ndipo alipoanza kuzunguka ili kuangalia uwezekano kama anaweza kumuona Mary.

Tayari alishachorewa ramani ya kwenda nyumbani kwao, alifuata kinjia kinachoteremka bondeni kidogo, lakini unavunja kijito kidogo cha maji kwa kukiruka tu, unapandisha juu kidogo ndipo unapoikuta nyumba yao.

Alikifuata kinjia hicho. Kila kitu kilikuwa ni kama alivyoelekezwa. Aliiona nyumba ambayo aliambiwa kuwa ingekuwa ndiyo kwa kina Mary. Alizuga kama hana mpango napo kabisa na lengo ilikuwa ni kupita tu.

Wakati anaipita nyumba, alimuona kwa mbali Mary akiwa anamwaga maji kwenye sufuria na alipogeuka kutaka kurejea ndani macho yaligongana.

Adel alidondosha macho yake haraka na kuendelea na safari yake kama anapita tu hakuwa na mpango wowote ule.

Tayari akili yake ilimtuma atembee kwa kiasi cha robo saa hivi halafu ageuke na kurejea, kwani alipotaka kufika tayari amepaona.




**"Pole sana Adel, hata mimi naona hali uliyoipata baada ya kukwambia hivyo, ndiyo maana mimi sikutaka kukwambia, nilijua tu haya, utahuzunika na kusikitika, wewe ni shujaa wangu ujue."**

Dakika tano tu baadaye alisikia vishindo vya miguu, ni kama mtu anakimbia nyuma yake au anamkimbilia. Kabla hajageuka akasikia sauti "Mgeni Mgeni". Akageuka. Alikuwa ni Mary. Inavyookena alivyomuona aliingia ndani tu na kuweka sufuria, akaanza safari ya kumfuata.

Alikuwa amevaa khanga tu ya nyumbani na nyingine akiwa amejitanda.

Akapunguza mwendo alipomkaribia. Adel alibaki amesimama tu akimuangalia. Hakuonyesha tabasamu wala hasira.

"Samahani mgeni, najua nimekukwaza jana nilikwambia kuwa nitakuja kwenu." Akajitetea. Hakujibiwa kitu.

"Umekasirika sana, samahani, siyo kosa langu kuna wageni walikuja jana nyumbani, kwa hiyo mimi ilibidi niwe mpishi, ndiyo maana ukaona kimya." Akazidi kujitetea.

"Unaendeleaje?" Ilikuwa ni kauli ya kwanza ya Adel kwa binti huyo. Ndipo alipokumbuka kuwa anaulizwa hivyo kwa sababu tangu lile tukio la kukoswakoswa na bodaboda na yeye kumuokoa hawajaonana.

"Naendelea vizuri tu mtu wangu, nisamehe mwenzio."

"Hayo yamepita, achana nayo, tuongeee mengine."

"Haya, nakusikiliza."

"Mary, najua wewe ni mrembo sana na wanaume siyo kijiji hiki tu, kila mmoja angetamani kuwa na wewe, je una mpenzi au mchumba?"

"Kwa nini umeuliza hilo swali?"

"Wewe unajua kwa nini nauliza hivyo, nataka uwe wangu."

Ni maneno yaliyotengeneza tabasamu pana kwa Mary.

"Kusema kweli tangu siku ya kwanza nilipokuona kwenye ule mkutano wenu wa kijiji na yule mwekezaji wenu, nimetokea kukupenda sana. Na jana tulipokutana hadi kuponyeka kwenye ajali ya bodaboda kabla na baada, nilionekana kufarijika kuwa na mtoto mzuri kama wewe."

"Mmmh muongo wewe mgeni."

"Mimi kwa sasa siyo mgeni, nina wiki na nusu hapa kwenu, niite Adel, hilo ndiyo jina langu. Ila tu mimi si muongo kama unavyodhani."

Waliangaliana kila mmoja ni kama alikuwa anamtathmini mwenzake. "Nimekuuliza swali hujanijibu, una mpenzi au mchumba hapa kijijini?"

"Ni...ninae ndiy...o" Akajibu Mary kwa kigugumizi.

Mshtuko wa moyo kwa mbali ukampiga Adel. Kama mwanaume, pamoja na kwamba alijua msichana kama yule hawezi kukosa mwanaume, lakini wivu ulimshika ghafla.

"Mpenzi au mchumba?"

"Mchumba." Lilikuwa jibu baya zaidi kuliko la mwanzo.

"Amekutolea barua nyumbani kwenu?"

"Nd...iy...o" Akajibu kwa unyonge zaidi.

Ni kama msichana huyo hakutaka kumuumiza Adel. Lakini akalazimika kumwambia ili baadaye usitokee mtafaruku.

"Anaitwa nani?" Lilikuwa swali lisilokuwa na maana yoyote ile, lakini lilimtoka kwa wivu na hasira iliyojificha."

Hata kama akijua jina ingemsaidia nini? Hata yeye mwenyewe alitambua kuwa swali lake halikuwa na maana yoyote.

"Enock." Akajibiwa.

"Yupo hapa hapa kijijini?"

"Ndiyo na ndiyo maana jana nilikwambia usije nyumbani kwa sababu huwa anakuja mara kwa mara na watu wote kijijini wanafahamu hilo. Hapa yenyewe kama akitokea mtu akatuona na kwenda kumwambia itakuwa kasheshe, ndiyo maana mimi jana nilitaka kuja kwa siri, na hapa nimejiiba tu."

Majibu hayo yote yalimfanya Adel kushusha pumzi ndefu na kuwa mpole ghafla hali ambayo hata Mary hakupata shida kuitambua.

"Pole sana Adel, hata mimi naona hali uliyoipata baada ya kukwambia hivyo, ndiyo maana mimi sikutaka kukwambia, nilijua tu haya, utahuzunika na kusikitika, wewe ni shujaa wangu ujue."

"Mary, nikwambie kitu, kama ungeuona moyo wangu umeumia na kuvunjika sana. Ukweli tu ni kwamba nilitokea kukupenda ghafla kutoka ndani kabisa ya moyo wangu. Naheshimu maamuzi yako. Naheshimu muda, ni kwamba kuna mtu amewahi mimi nilichelewa, lakini nikwambie tu, nakupenda sana na nitaendelea kukupenda." Wakati anaongea maneno hayo machozi yalianza kumtoka Adel. Mwanamke hakuvumilia. Akatoa khanga aliyojitanda na kuanza kumfuta machozi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KOCHA COASTAL AFUNGUKA ALIPOWASHIKA PRISONS

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Yusuph Chipo amesema haikuwa kazi rahisi kuifunga timu ngumu ya Prisons, badala yake aliamua kubadilisha mfumo wa kuchezesha mabeki sita kwa ajili ya kuwadhibiti washambuliaji wenye nguvu wa timu hiyo.

Akizungumza baada ya kupata ushindi wa ugenini wa mabao 2-0 dhidi ya Prisons Uwanja wa Sokoine Mbeya, kocha huyo raia wa Kenya alisema ilifanyika kazi ya kuifunga timu hiyo kwa sababu waliweka washambuliaji wawili wenye nguvu na mawinga wao walikuwa wakifanya kazi ya kupiga krosi na mabeki kupiga mipira mirefu kitu ambacho kiliwapa tabu sana mabeki wake.

"Prisons walileta mastraika wawili ili mipira yote ipigwe ndani, ndiyo maana na sisi ilibidi tutafute mlinzi mmoja tumuongeze ili aende kuwasaidia wenzake kupiga vichwa mipira ile mirefu. Nilimwingiza kiungo wangu wa kukaba ili akawasaidie wenzake pale, na viungo waliobaki niliwaambia kazi yao itakuwa ni kuiokota mipira yote itakayodondoka baada ya mapambano ya kugombea mipira ya juu," kocha huyo alifichua siri hiyo.

**Alisema mara nyingi mpira mi mifumo na ujanja, ikiwemo kubadilika baada ya kuona nguvu ya mpinzani ilipo.**

Yalikuwa ni mabao ya Maabad Maulidi dakika ya nne na Hamadi Majimengi dakika ya 60.

Unakuwa ni ushindi wa tatu kwa Coastal Union, lakini pia Prisons ikipoteza mara ya tatu pia kwenye mechi hiyo.

Kwa matokeo hayo, Coastal Union inapaa hadi nafasi ya 11 kwa pointi 11, ikicheza mechi nane, Prisons baada ya kupoteza bado ipo juu kwenye nafasi ya nane kwa pointi zake 14, ikicheza mechi 11 mpaka sasa.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kushoto) akikabidhiwa picha maalumu ya Rais, Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa iliyoandaliwa na wasanii walioshiriki Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo lililofanyika katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), mkoani Pwani jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# *Klabu zapewa changamoto viingilio vya mechi*

**Na Hadija Mngwai**

KLABU za Ligi Kuu Bara zimetakiwa kufanya tathimini ya viingilio vya mechi zao ili kuweza kuwavutia mashabiki kuingia uwanjani kutokana na upungufu wa mashabiki uliopo hivi sasa na kupelekea changamoto ya ukosefu wa mapato kwa klabu.

Maamuzi hayo yamefanyika katika mkutano wa tisa wa Baraza Kuu la Bodi ya Ligi Kuu Bara uliofanyika juzi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Kuu Bara, Almas Kasongo amesema kuwa, katika mkutano huo kuna mambo mbalimbali ambayo yamejadiliwa likiwemo suala la upungufu wa mashabiki viwanjani kunakochangia kupungua kwa mapato kwa vilabu.

"Kikao kimezungumza mambo mengi kwa mapana na marefu na mambo mbalimbali kwa upana wake, lakini tumezungumza kuona jinsi ya kuongeza mapato na pia vilabu vinatakiwa watoke huku, asilimia kubwa ya klabu zinategemea mapato kutoka vyanzo vya Bodi ya Ligi na TFF.

" Kwa hiyo tumekubaliana kwa nia njema kabisa klabu ziweze kutoka na kutafuta vyanzo vingine vitakavyowasaidia katika uendeshaji wa shughuli zao, pia tumekubaliana vilabu viweze kurudi katika ofisi zao na kupunguza viingilio kwa kuvishusha ili kuvuta watazamaji waweze kuja kutazama mechi zetu.

"Pia tumekubaliana kufanya kazi ya kisayansi kwa kutafuta mshauri aweze kutufanyia hiyo kazi kwa kuona sababu ya watu kupungua katika michezo ya Ligi Kuu, kuna sababu tofauti ambazo tunazipata lakini hatupati sababu ya kisayansi kwa nini watu hawaji viwanjani.

"Bahati nzuri tumeshea mapato yote ya vilabu na kuona kila timu imeingiza kiasi gani katika mechi zao katika viwanja vyao, hivyo tumekubaliana kurudi kwenye vilabu na kufanya tathimini ya viingilio vyetu na tufanye hamasa kubwa kadri inavyowezekana tuweze kuwavutia watazamaji wetu," alisema Kasongo..

## Semina ya kimataifa Karate kufanyika Tz

**Na Saada Akida**

WAKATI serikali ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ikiwekeza katika michezo, nchini imepata nafasi nyingine ya kuwa mwenyeji wa kuendesha semina ya kimataifa ya mchezo wa Karate.

Semina inatarajiwa kuanza rasmi Desemba 31, 2022 hadi Januari 4, 2023 na washiriki kufanya mtihani siku ya mwisho kwa madaraja ya mikanda tofauti.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa West Coast Shotokan Karate Tanzania, Sensei Anastasius Liwewa ambaye yuko daraja la tano mkanda mweusi alisema semina hiyo inafanyika kila mwaka na sasa ni mwaka wa saba kufanyika Tanzania.

Alisema Semina hiyo itaendeshwa na mkufunzi wa kimataifa wa mchezo wa karate, Shihan Shalom Avitan kutoka Israel ambaye pia ni rais wa West Coast Shotokan Karate duniani.

"Hii semina itakuwa maalum kwa washiriki wa mchezo wa karate kutoka ndani na nje ya nchi, itafanyika Zanzibar kwa siku mbili na tatu itaendelea Tanzania Bara na siku ya mwisho kutakuwa na mitihani ya washiriki.

"Tunaamini kufanya hivyo ni kuendeleza sera ya Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari wa mbele katika kusimamia michezo hapa nchini kuwa imara na kujitangaza kwa kufanya vizuri," alisema Liwewa.

Alisema katika kusimamia misingi ya rais, wamemualika mkufunzi huyo ambaye anatarajia kutua nchini Novemba 29, mwaka huu kwa kutoa mafunzo hayo na baadae kusimamia mitihani.

## Mashindano ya karate miaka 6 kurindima

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Vijana wenye umri kuanzia miaka 6 ya mchezo wa Karate yanatarajiwa kufanyika Novemba 13 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, mwenyekiti wa Tawoska, Levina Tarimo alisema mashindano hayo yatashirikisha klabu zote za mkoa wa Dar es Salaam.

"Haya mashindano yatashirikisha Klabu zote za mkoa wa Dar es Salaam, tunaomba mashabiki wake kwa wingi kuona vipaji," alisema Tarimo.

Alisema lengo la mashindano hayo ni kumpata bingwa wa mwezi ambaye hupatikana kila mwezi.

"Kila mwezi huwa tunatafuta bingwa wa mwezi tunafanya hivi ili wachezaji wazidi kuonesha viwango vyao," alisema.

Alisema mashindano yatashirikisha wanaume na wanawake na watacheza kwa mifumo tofauti.

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM KUBAKI

KLABU ya Borussia Dortmund ina imani kuwa wanaweza kumbakisha kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19 hadi mwisho wa msimu huu, licha ya klabu kadhaa kama Chelsea, Liverpool, Manchester City na Manchester United kumuwinda. (*90Min)*

### FELIX ATAKIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid, Joao Felix na mabingwa hao wa Ufaransa wanaweza kujaribu kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 23 kwa mkopo wakati wa dirisha la Januari. (*Le Parisien, via Marca*)

### ROMA WAMTAKA BELLERIN

AS Roma wataelekeza mawazo yao kwa beki wa kulia wa Barcelona, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 27, wakati huu ambao Diogo Dalot wa Ureno mwenye miaka 23, waliyekuwa wanamfuatilia akionekana sehemu muhimu ya mipango ya Manchester United. (*Calciomercato)*

### MANE KUPELEKWA KWA WAGANGA

SENEGAL itatumia waganga wa kienyeji katika jaribio la kumsaidia mshambuliaji wa Bayern Munich, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30 apone jeraha kwa wakati ili acheze Kombe la Dunia. *(Mail)*

### DAVIES KUWA FITI

MLINZI wa Canada, Alphonso Davies anaamini atakuwa fiti kwa Kombe la Dunia baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kupata majeraha ya msuli wa paja wakati akiichezea Bayern Munich dhidi ya Hertha Belin Jumamosi iliyopita. (*Mail)*

### CALVERT-LEWIN KUCHUNGUZWA

MSHAMBULIAJI wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 25 ataonana na mtaalamu ili kujua ukubwa wa tatizo lake la bega lililoteguka. (Guardian)

### VILLA YASAKA MSHAMBULIAJI

KLABU ya Aston Villa inasaka mshambuliaji mkubwa katika dirisha la uhamisho la Januari, wakati mlinzi wa Villarreal, Pau Torres mwenye umri wa miaka 25 pia anavutiwa na kocha aliyeteuliwa hivi karibuni, Unai Emery. (*Football Insider)*

### SPURS YATAKA BEKI, STRAIKA

KLABU ya Tottenham Hotspur itaweka kipaumbele kwa beki wa kulia anayecheza kama winga na mshambuliaji wa akiba katika dirisha la usajili la Januari. (*90Min*)

### DEPAY KURUHUSIWA

BARCELONA inaweza kumruhusu mshambuliaji wake raia wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28 kuondoka katika dirisha la usajili la Januari. (*Caughtoffside*)

### SOUTHAMPTON KULIPA FIDIA

KLABU ya Southampton itailipa klabu ya ligi daraja la kwanza, Luton Town zaidi ya pauni milioni 4 kama fidia kwa ajili ya kocha Nathan Jones, ambaye alitangazwa kuchukua nafasi ya Ralph Hasenhuttl aliyetimuliwa Saints Alhamisi. *(Telegraph*)

### PIQUE NA URAIS

MLINZI wa zamani, Gerard Pique amesema atawania urais wa Barcelona miaka michache ijayo baada ya kustaafu soka wiki hii. (*ESPN*).

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOUTHGATE: MAGUIRE BEKI BORA WA ENGLAND

**Atetea kumteua kwenda nae kombe la Dunia, asisitiza uzoefu unambeba kuliko vijana ambao...**

**LONDON,** England

GARETH Southgate amesema Harry Maguire ni mmoja wa "mabeki bora wa kati" wa England baada ya mlinzi huyo kutajwa miongoni mwa kikosi cha Simba Watatu hao kinachokwenda nchini Qatar kwa Kombe la Dunia.

Nahodha huyo wa Manchester United ataelekea kwenye michuano yake ya tatu mikubwa akiwa na timu ya taifa, baada ya ile ya Urusi 2018 na Euro 2020, licha ya kuwa na wakati mgumu wa kupata namba kikosi cha kwanza klabuni kwake.

Maguire ni mmoja wa wachezaji waliokuwa na kiwango cha kuvutia kwenye kikosi kilichofika nusu fainali miaka minne iliyopita, na amekuwa akiichezea England mara kwa mara chini ya Southgate.

Uzoefu huo katika mechi kubwa za mtoano umemsaidia kushika nafasi yake licha ya kushindwa kuitumikia United, huku kujumuishwa kwake kunaonyesha uungwaji mkono mkubwa anaoupata kutoka kwa Southgate.

**"Yeye ni mmoja wa mabeki wetu bora wa kati," alisema. "Nadhani ndani ya kikosi, tuna wachezaji wengi ambao wamekuwa kwenye mashindano, wa mecheza kwa kiwango hicho, na wanajua kinachohitajika.**

"Tuna wachezaji wengine ambao wanacheza vizuri, ambao wako katika kiwango kwa sasa, na lazima tusawazishe yote hayo wakati wa kuchagua timu yetu."

Kuchaguliwa kwa Maguire kulitarajiwa, lakini kumezua taharuki baada ya kuachwa kwa wachezaji wanaochikupukia kama Fikayo Tomori wa Milan na Marc Guehi wa Crystal Palace.

Southgate alipendekeza kwamba, licha ya fursa chache za Maguire, wapinzani wake wachanga hawakuonesha viwango vya kutosha kuondosha imani yake kwa Maguire na wengine, kama vile mchezaji anayecheza kwa mkopo pale Everton, Conor Coady.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,048,8

MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
IHEFU FC
1 | 1.23
X | 5.40
2 | 13.00

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# PIQUE AFIKIRIA URAIS BARCELONA

**BARCELONA,** Hispania

GERARD Pique amedokeza kuwa atawania urais wa Barcelona katika siku zijazo lakini kwa sasa "atazingatia mambo mengine" mara tu baada ya kustaafu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alitangaza rasmi kutundika daruga zake, baada ya kutwaa mataji nane ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Ligi ya mabingwa Ulaya mara tatu, kombe la Euro na la Dunia.

Akiwa amekuzwa akiwa Barcelona, Pique aliingizwa katika kikosi cha kwanza baada ya kuitumikia Manchester United kwa miaka minne na kuwa tegemeo katika kipindi cha miaka 14.

Tofauti na wachezaji wenzake wa zamani Xavi na Andres Iniesta, Pique hana mpango wa kuingia kwenye ukocha, lakini amebainika kuwa urais wa klabu ni jambo la kuzingatia katika siku zijazo.

"Nina uhakika itanivutia wakati mmoja, lakini sio sasa hivi," alisema Pique akiiambia Ibai Llanos.

"Kutofanya mazoezi kila siku kutanipa fursa ya kuzingatia mambo mengine. Katika siku zijazo, tutaona, lakini ningependa kuisaidia klabu ya maisha yangu kuongeza uwezo nilionao."

Pique hakuweza kushiriki katika ushindi wa katikati ya wiki dhidi ya Osasuna, baada ya kuoneshwa kadi nyekundu kama mchezaji wa akiba wakati wa mapumziko, lakini aliaga Camp Nou katika ushindi wa 2-0 dhidi ya Almeria hapo awali.

Kutolewa huko kulimaanisha mengi kwa beki huyo, ambaye alieleza kuwa amekuwa akifikiria kustaafu katika kipindi chote cha miezi michache ya kwanza ya msimu huu.

# Deschamps: Benzema atakuwa fiti Kombe la Dunia

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps amedai kuwa Karim Benzema 'analipa gharama' kwa kucheza sana miaka ya hivi karibuni baada ya kusumbuliwa na majeraha hadi sasa msimu huu, lakini ana imani fowadi huyo wa Real Madrid atakuwa fiti kwa wakati kwa mechi ya kwanza ya Les Bleus hao kwenye Kombe la Dunia.

Benzema hakuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa kilichonyanyua taji la Kombe la Dunia 2018 kwa sababu ya kutoshiriki kwa muda mrefu katika majukumu ya kimataifa baada ya kashfa yake ya kuvujisha mkanda wa video ya ngono ya mchezaji mwenzake mwaka 2015.

Lakini aliitwa tena na Deschamps kwenye Euro 2020 mwaka jana, kabla ya kuwa na msimu bora zaidi wa maisha yake yote akiwa na Real, akishinda LaLiga, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ballon d'Or.

Benzema amefunga takribani bao moja kwa kila mechi kwenye LaLiga msimu huu, lakini matatizo ya misuli na uchovu vimemfanya afikishe mechi saba pekee za nyumbani, huku akiwa hajafunga kabisa katika mechi nne za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa Los Blancos hao.

"Anajua kuwa Kombe la Dunia ni wakati muhimu sana kwake. Atafanya kila kitu, kama kundi zima, kuwa tayari Novemba 22," alisema Deschamps akiiambia TF1.

"Kuna kipindi Benzema alicheza sana na sasa analipa gharama kutokana na majeraha madogo. Lakini anajua Kombe la Dunia ni muhimu."

Deschamps pia alikanusha mapendekezo kwamba kukosekana kwa Benzema hivi karibuni kwa Real Madrid kumekuwa ni jaribio la makusudi la kujiokoa ili aitumikie Ufaransa.

"Sio kwamba Benzema hakutaka kuichezea Real Madrid, hakuwa tayari. Lakini nina uhakika atakuwa tayari kwa Kombe la Dunia," aliongeza kocha huyo.



375,802/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Crystal Palace | 3.04 | 3.19 | 2.37 |
| 02. 12/11/22 | 18:00 | Bristol City vs Watford | 2.89 | 3.39 | 2.36 |
| 03. 12/11/22 | 18:00 | Bournemouth vs Everton | 2.78 | 3.23 | 2.53 |
| 04. 12/11/22 | 18:00 | Huddersfield vs Swansea | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 05. 12/11/22 | 18:00 | Preston vs Millwall | 2.41 | 3.13 | 3.03 |
| 06. 12/11/22 | 18:00 | Coventry vs QPR | 2.36 | 3.22 | 3.02 |
| 07. 12/11/22 | 20:00 | Basaksehir vs Galatasaray | 2.42 | 3.40 | 2.80 |
| 08. 12/11/22 | 20:00 | Sampdoria vs Lecce | 2.54 | 3.08 | 2.89 |
| 09. 12/11/22 | 20:00 | FC Sion vs St. Gallen | 2.80 | 3.60 | 2.37 |
| 10. 12/11/22 | 20:30 | Newcastle vs Chelsea | 2.32 | 3.34 | 2.99 |
| 11. 12/11/22 | 22:45 | Bologna vs Sassuolo | 2.38 | 3.34 | 2.89 |
| 12. 13/11/22 | 14:30 | Atalanta vs Inter | 2.90 | 3.54 | 2.29 |
| 13. 13/11/22 | 16:15 | FC Zurich vs Servette Geneva | 2.37 | 3.30 | 2.95 |
| 14. 13/11/22 | 17:00 | Istanbulspor vs Hatayspor | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 15. 13/11/22 | 17:00 | Kayserispor vs Konyaspor | 2.58 | 3.28 | 2.68 |
| 16. 13/11/22 | 17:00 | Montpellier vs Reims | 2.45 | 3.38 | 2.73 |
| 17. 13/11/22 | 17:30 | Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.44 | 3.41 | 2.72 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 12/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1254 | Dinamo Brest vs Slutsk | 1.78 | 3.35 | 4.18 |
| 15:30 | 2638 | St Mirren vs Rangers | 6.97 | 4.68 | 1.39 |
| 15:30 | 2677 | Manchester City vs Brentford | 1.16 | 6.83 | 14.52 |
| 16:00 | 5450 | Mtibwa Sugar vs Azam | 3.60 | 2.83 | 2.13 |
| 17:00 | 2658 | Lokomotiva Zagreb vs Istra | 1.78 | 3.50 | 3.98 |
| 17:00 | 3790 | Napoli vs Udinese | 1.46 | 4.54 | 5.72 |
| 17:00 | 3945 | Fenerbahce vs Giresunspor | 1.29 | 5.35 | 8.92 |
| 17:00 | 4084 | Banik Ostrava vs Bohemians | 2.19 | 3.58 | 3.08 |
| 17:00 | 4558 | Mladost Lucani vs Kolubara | 2.06 | 3.35 | 3.16 |
| 17:30 | 1763 | Hertha BSC vs FC Koln | 2.18 | 3.52 | 2.97 |
| 17:30 | 1800 | Augsburg vs VfL Bochum | 2.14 | 3.42 | 3.12 |
| 17:30 | 2031 | Werder Bremen vs RB Leipzig | 3.67 | 3.91 | 1.81 |
| 17:30 | 2095 | Hoffenheim vs VfL Wolfsburg | 2.17 | 3.56 | 2.97 |
| 17:30 | 5482 | Bayer Leverkusen vs Stuttgart | 1.69 | 3.97 | 4.26 |
| 18:00 | 1026 | CD Fuentes vs Osasuna | 35.02 | 15.01 | 1.02 |
| 18:00 | 1901 | Celtic vs Ross County | 1.08 | 9.33 | 22.84 |
| 18:00 | 2330 | West Ham vs Leicester | 2.05 | 3.31 | 3.46 |
| 18:00 | 2405 | Nottingham vs Crystal Palace | 2.93 | 3.12 | 2.39 |
| 18:00 | 2435 | Bournemouth vs Everton | 2.77 | 3.11 | 2.52 |
| 18:00 | 2742 | Liverpool vs Southampton | 1.22 | 6.34 | 9.90 |
| 18:00 | 3311 | UD Barbadas vs Valladolid | 59.84 | 15.96 | 1.01 |
| 18:00 | 3355 | Arbroath vs Cove Rangers | 2.01 | 3.35 | 3.45 |
| 18:00 | 3589 | Hearts vs Livingston | 2.01 | 3.44 | 3.49 |
| 18:00 | 4030 | Tottenham vs Leeds | 1.60 | 4.06 | 4.75 |
| 18:00 | 5672 | St Johnstone vs Motherwell | 2.50 | 3.15 | 2.80 |
| 18:00 | 5991 | Morton vs Partick Thisle | 2.42 | 3.30 | 2.71 |
| 18:30 | 3656 | FC Volendam vs Utrecht | 3.42 | 3.86 | 1.89 |
| 19:00 | 1542 | TSV Hartberg vs Rapid Vienna | 4.08 | 3.74 | 1.70 |
| 19:00 | 1906 | Lens vs Clermont Foot | 1.41 | 4.57 | 6.76 |
| 19:00 | 4219 | Boluspor vs Yeni Malatyaspor | 1.71 | 3.60 | 4.19 |
| 19:00 | 4478 | Simba vs Ihefu FC | 1.23 | 5.40 | 13.00 |
| 19:30 | 3534 | Lokomotiv Moscow vs Spartak Moscow | 3.82 | 3.62 | 1.85 |
| 19:30 | 4123 | Slaven Belupo vs Hajduk Split | 4.30 | 3.47 | 1.73 |
| 20:00 | 1262 | Sampdoria vs Lecce | 2.56 | 2.95 | 2.85 |
| 20:00 | 2683 | FC Sion vs St. Gallen | 2.64 | 3.48 | 2.45 |
| 20:00 | 5973 | Basaksehir vs Galatasaray | 2.73 | 3.37 | 2.43 |
| 20:30 | 2648 | Autol vs Mallorca | 59.73 | 17.92 | 1.01 |
| 20:30 | 3742 | Newcastle vs Chelsea | 2.28 | 3.28 | 2.98 |
| 20:30 | 4051 | Queens Park vs Inverness | 2.18 | 3.40 | 3.01 |
| 20:30 | 5743 | Schalke 04 vs Bayern Munchen | 12.90 | 7.94 | 1.14 |
| 20:45 | 5702 | Emmen vs Ajax | 8.12 | 5.55 | 1.29 |
| 21:00 | 2595 | Aberdeen vs Dundee Utd | 1.72 | 3.68 | 4.48 |
| 22:30 | 2029 | Grasshoppers vs FC Basel | 3.00 | 3.65 | 2.14 |
| 22:45 | 3559 | Wolverhampton vs Arsenal | 5.45 | 3.85 | 1.57 |
| 22:45 | 3752 | Bologna vs Sassuolo | 2.28 | 3.41 | 2.87 |
| 23:00 | 1067 | CD Rincon vs Espanyol | 59.79 | 15.94 | 1.01 |
| 23:00 | 1734 | Santa Amalia vs Villarreal | 29.96 | 19.97 | 1.01 |
| 23:00 | 4176 | PSV Eindhoven vs AZ Alkmaar | 1.51 | 4.47 | 5.16 |
| 23:00 | 5778 | Rennes vs Toulouse | 1.48 | 4.46 | 5.75 |
| 23:30 | 3708 | Boavista vs Porto | 8.17 | 4.78 | 1.34 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SERIKALI YATOA NENO ADHABU ZA NIDHAMU LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

HUKU wimbi la adhabu kwa wanamichezo likikithiri, serikali imesisitiza nidhamu katika michezo mbalimbali hususani kwa wachezaji wa mpira wa miguu.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu katibu mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Said Yakubu katika mkutano mkuu wa bodi ya Ligi Kuu ya Tanzania (TPLB), uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Yakubu alisema serikali imekuwa ikishuhudia mambo mbalimbali ya utovu wa nidhamu na adhabu zinazotolewa kwa lengo la kupunguza utovu wa nidhamu katika michezo.

Alisema licha ya adhabu hizo kutolewa kama funzo kwa wale wanaovunja sheria za soka, haamini kama ni chanzo cha TPLB kujipatia mapato, ingawa alisisitiza kutafutwe namna nzuri zaidi ya kuondokana na matukio hayo.

"Utafutwe ufumbuzi zaidi na kuongeza umakini, kuhakikisha nidhamu inakuwa kubwa ili soka letu liwe kioo dhidi ya nchi nyingine, yapunguzwe matukio ya kuondoa sintofahamu kwa wadau wa soka ndani na nje.

"Siamini kujengwa kwa magereza mengi ndio suluhisho la kuondoa vibaka wengi mtaani, bali ni kutoa elimu ya kuwafanya waondokane na nidhamu mbovu, natoa wito kwa wachezaji, viongozi wa ngazi zote na makocha wazingatie kanuni zilizopo kwa lengo la kuondoa matukio yasiyofaa," alisema Yakubu.

Mbali na hilo aligusia uwepo wa wachezaji wengi wa kigeni wanaokuja nchini kwani wanatakiwa kuwa na tija ya kuzisaidia timu zilizowasajili, na waendane na thamani ya malipo yao kama zilivyo klabu za nje.

"Wapo mastaa wakubwa Ulaya wanaolipwa fedha nyingi wanaposajiliwa nje ya nchi zao na wanachokifanya kinaonekana, hapa kwetu sijui kama hilo linazingatiwa. Kwa msimu mzima mchango wao unakuwa asilimia 30 na hiyo inawanyima fursa wazawa ambao watalisaidia taifa lao na yapo mambo yanayopaswa kuangaliwa zaidi ikiwemo kuleta mchezaji anayetegemewa katika taifa lao," alisema.

Aliongeza kwa kuwataka Bodi kuangalia mambo mengi ya kujenga soka, kutokana na chombo hicho kuwa na dhamana kubwa, utendaji wa waamuzi kwa kulalamikiwa na baadhi ya timu na wengine kufungiwa waamuzi kwa sababu ya kutofuata sheria za soka hasa wanapochezesha timu kubwa.



Vijana wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi ya mpira wa Kikapu katika viwanja vya michezo vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Hasira za Simba kwa Ihefu leo*

INATOKA UK 32

Nahodha msaidizi wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala' alisema kuwa wamejiandaa vizuri na hawatoidharau Ihefu kwa sababu inaburuza mkia, akisema kuwa ina wachezaji wazuri na timu yao ni nzuri pia.

Kocha msaidizi wa Ihefu, Themi Felix alisema mbali na kushika mkia, lakini leo watawaonyesha kitu tofauti licha ya kwamba Simba ni timu kubwa na bora.

"Kwa asilimia kubwa maandalizi tumeyamaliza, na kwa kweli kwa mechi za karibuni timu yetu imebadilika, tatizo letu ni kutumia nafasi tu zinazopatikana," alisema.

Kwenye mechi ya leo, Ihefu, yenye pointi tano ikishika nafasi ya mwisho kwa mujibu wa kocha huyo, itawakosa Juma Nyosso ambaye ana kadi nyekundu, Andrew Senchimba, Joseph Kimwaga na Joseph Kinyozi.

## Simba Queens, Bayelsa mechi ya heshima CAF

INATOKA UK 32

"Tunashukuru Mungu kwa hatua tuliyofika, malengo yetu makuu kwa msimu huu yalitimia, kesho (leo) tutashuka uwanjani kupambana kusaka ushindi, tunamuomba Mungu atuamshe salama ili kukamilisha kazi iliyotolewa," alisema mshambuliaji huyo.

Aliongeza anaamini benchi la ufundi litafanyia kazi mapungufu waliyoyabaini kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya mwakani na msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambao utafanyika kuanzia Desemba 5, mwaka huu.

Simba Queens ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania watafungua pazia la ligi hiyo kwa kuwakaribisha JKT Queens kwenye Uwanja wa Mo Arena wakati itakutana na watani zao, Yanga Princess ifikapo Desemba 16, mwaka huu.

Wakati huo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez ameongeza zawadi ya Sh. Mil 30 wakishinda mechi ya kesho na hivyo watapewa jumla Sh Mil 130, kwani awali ilikuwa imetoka ahadi ya Sh. 100 kama wakitinga nusu fainali.

Michezo
Jumamosi Novemba 12, 2022
Nipashe



Southgate: Maguire beki bora wa England

UKURASA 29



Wachezaji wa Yanga wakishuka kwenye ndege katika Uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana, kutoka nchini Tunisia walikokwenda kucheza mchezo wa marudiano wa kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, CAF, dhidi ya Club Africain ya huko. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA:YANGA.**

# HASIRA ZA SIMBA KWA IHEFU LEO

## ●●● Yasaka pointi tatu muhimu, ikitoka kulazimishwa sare na Singida Big Stars...

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA kwenye nafasi ya tatu ya msimamo wa ligi kwa sasa na pointi zake 18, Simba leo saa moja usiku kwa saa za Afrika Mashariki, itashuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza mechi ya raundi ya 10 dhidi ya timu inayoshikilia mkia Ihefu.

Simba itaingia uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kuvutwa mkia, ikilazimishwa kutoka sare ya bao 1-1, Jumatano iliyopita dhidi ya Singida Big Stars kwenye Uwanja wa Liti, Singida na kushindwa kuiengua Yanga kileleni.

Iwapo itashinda mechi ya leo itakwenda juu kileleni na kufikisha pointi 21, vinginevyo itabaki hapo kwani hata ikitoka sare itakuwa na pointi 19 wakati Yanga na Azam zote zina pointi 20 hadi sasa.

**Kaimu Kocha Mkuu wa Simba Juma Mgunda amesema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na wanaelewa malengo na kiu ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo na kutaka kushinda mchezo huo.**

"Maandalizi yako vizuri na tuko tayari kupambana na Ihefu. Tulitoka sare na Singida Big Stars, unapokuwa hushindi kunakuwa na ugumu wa kufikia malengo tunaelewa hilo. Siku zote huwa napenda kusema ukweli ligi hii ni ngumu, naamini hata mchezo wa kesho (leo) utakuwa mgumu, haijalishi timu hiyo inashika nafasi ya ngapi. Na sisi Simba hatuidharau timu hiyo tutapambana kadri ya uwezo wetu ili kupata ushindi," alisema Mgunda.

Alisema kwenye mechi hiyo, mbali na Clatous Chama ambaye ana adhabu ya kutocheza mechi tatu, wengine ni Jimson Mwanuke na Israel Mwenda ambaye tayari ameanza mazoezi na Peter Banda aliyeumia kwenye mechi iliyopita dhidi ya Singida Big Stars.

Alisema alichokuwa akiwasisitiza wachezaji wake ni kutumia nafasi zinazopatikana kwani ni ukweli usiopingika kuwa timu inatengeneza nafasi nyingi, lakini haizitumii ipasavyo.

INAENDELEA UK 31

## Simba Queens, Bayelsa mechi ya heshima CAF

**Na Somoe Ng'itu,** RABAT

KIKOSI cha Simba Queens kinatarajia kukutana na Bayelsa Queens kutoka Nigeria katika mechi ya kusaka mshindi wa tatu itakayochezwa leo kuanzia saa 4:00 usiku kwa saa za Tanzania kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan jijini hapa.

Simba Queens ilishindwa kutinga fainali za mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake baada ya kufungwa bao 1-0 na mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns Ladies wakati Bayelsa Queens wao walipoteza mchezo wao dhidi ya ASFAR FC ya Morocco.

Bila kujali matokeo yoyote yatapatikana katika mechi ya leo, Simba Queens na Bayelsa Queens kila moja itapokea zawadi ya Dola za Marekani 200,000 wakati mshindi wa pili wa michuano hiyo atajinyakulia Dola za Marekani 250,000 na bingwa atapata kitita cha Dola za Marekani 400,000.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, aliliambia gazeti hili baada ya kushindwa kutimiza ndoto za kutwaa ubingwa wa Afrika, sasa anahitaji kuona wanarudi nyumbani na medali za mshindi wa tatu.

Lukula alisema watacheza mechi hiyo kwa nguvu ili kuwafuta machozi mashabiki wao na wadau wa soka wa Afrika Mashariki na Kati ambao walikuwa wanawawakilisha katika michuano ya mwaka huu.

"Tunataka kumaliza kazi kwa heshima, tunajua pia wapinzani wetu watahitaji ushindi ili kujifariji, mechi haitakuwa nyepesi, tuliumia kupoteza mchezo dhidi ya Mamelodi, sasa tunataka ushindi na kumaliza michuano kwa heshima," alisema Lukula.

Aliwataja wachezaji ambao ni majeruhi na hawako katika mipango yake kuelekea mechi ya leo ni mshambuliaji, Aisha Mnunka, Wema Maile na Zainab Ally.

Nahodha wa Simba Queens, Oppa Clement, alisema wachezaji wote wamejipanga kucheza kwa bidii na kuongeza wataingia uwanjani wakiwa wamesahau matokeo ya mchezo uliopita.

INAENDELEA UK 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >